

**ELIMU**
Andaeni mipango kulingana na mahitaji ya soko, katibu aambia TVETs **UK 3**



**DIJITALI**
Serikali, mashirika ya kijamii yaafikiana kuhamasisha umma kuhusu dijitali
**UK 6**


**UCHUMI**
KVDA yafadhili miradi ya ufugaji nyuki kuzima vita vinavyotokana na wizi wa mifugo



**UK 12**

www.mygov.go.ke
FEBRUARI 28, 2023
# MyGov.
TATHMINI YAKO YA WIKI
TOLEO No. 33/2022-2023

# Huduma zote za serikali kuwa za dijitali kufikia Juni- Waziri



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali (CS) Eliud Owalo akihutubu wakati wa ufunguzi rasmi wa Kongamano la Tatu la Nation kuhusu Dijitali mjini Mombasa.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali Eliud Owalo anasma kupitia tovuti ya e-citizen, huduma 839 tayari zimewekwa katika tovuti hiyo huku huduma 300 zikiwekwa kila wiki kufikia lengo la Juni 2023

**NA CHARI SUCHE NA SHAMIN MUSA (KNA)**

Serikali imetoa makataa iliyojiwekea ya Juni ambapo huduma zote za serikali zitakuwa zimewekwa katika tovuti ya e-Citizen. Hii itapiga jeki ushindani wa dijitali nchini.

Waziri wa Habari, Mawasi-

ENDELEA UK 2

## Takwimu za Wiki

**2**
Madaktari wa kutibu kansa ya maini waliopokea mafunzo kwa usaidizi wa Serikali ya Ufaransa

**889**
Idadi ya wanafunzi waliohitimu hivi majuzi kutoka Karumo Technical Training Institute

**5,000**
Huduma za serikali ambazo zitawekwa kwenye mtandao, kulingana na Katibu wa Uhamiaji na Huduma za Raia (PS) Julius Bitok.

**40,000**
Mabaharia serikali inapanga kuwaajiri kila mwaka kwa lengo la kutimiza 200,000 kufikia 2027.

**62.2B**
Kiasi cha pesa serikali imetumia kwa miaka mingi kugharimia bili za matibabu za walio na magonjwa ya kiakili.

**Sh250B**
Kiasi cha pesa ambacho Serikali imepata kwa ustawishaji wa viwanda

# Mpango mpya wa pensheni kunufaisha wastaafu nchini



**Wa pili kutoka kulia, mlezi wa Public Service Superannuation Scheme, John Matiangi, na Kamishna wa Kaunti ya Homa Bay Moses Lilan, afisini mwake hivi majuzi.**

**NA SITNA OMAR (KNA)**

Serikali, kupitia Wizara ya Fedha, imetekeleza mpango mpya wa pensheni utakaonufaisha watumishi wote wa umma na walimu wanapostaafu.

Mpango huo unaofahamika kama Public Service Superannuation Scheme (PSSS) ni sehemu ya mageuzi katika sekta Huduma ya Pensheni ya Umma iliyoanzishwa na serikali mwaka wa 2012 kupitia ilani katika gazeti rasmi Januari 1 2021.

Mpango huo unafaidi watumishi wa umma, walimu walioajiriwa na Tume ya Huduma ya Walimu (TSC) na maafisa wa usalama, wakiwemo Huduma ya Taifa ya Polisi, Huduma ya Magereza na Huduma ya Taifa ya Vijana.

Michael Obonyo, ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Habari anayesimamia kitengo cha mawasiliano katika Wizara ya Fedha alisema kwamba mpango huo utahakikisha uendelevu wa pensheni katika sekta ya umma.

Mpango wa awali uliofahamika kama - Defined Benefit Scheme, ulitegemea ufadhili kutoka kwa hazina kuu ya serikali.

"Kuanzishwa kwa mpango huu mpya sasa kumekomesha ufadhili kutoka kwa hazina kuu na hakikisho la pensheni endelevu katika utumishi wa umma," alisema.

PSSS kwa upande mwingine inatumia mbinu ya michango ambapo serikali na wafanyakazi watachangia mpango huo kila mwezi kufadhili marupurupu ya kustaafu ya wafanyakazi.

Mpango huo utanufaisha watumishi wa umma ambao wako na umri wa chini ya miaka 45 kuanzia Januari 1 2021 na ambao wameajiriwa kazi ya

ENDELEA UK 2

KOMESHA COVID-19
" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Huduma zote za serikali kuwa za dijitali kufikia Juni– Waziri

ENDELEA KUTOKA UK 1

liano na Uchumi Dijitali Eliud Owalo alisema kwamba Wizara yake inatekeleza Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Dijitali wa 2022-2032, kuwezesha vipaumbele vya dijitali vya nchi.

Owalo pia aliongeza kuwa mpango huo unahusu nguzo tano za kuongoza ajenda ya mabadiliko ya dijitali yanayojumuisha: muundo msingi wa dijitali, huduma za dijitali na usimamizi wa data, ujuzi wa data, ujasiriamali wa dijitali na mfumo kazi wa sera, kisheria na uthibiti.

Akizungumza katika uzinduzi rasmi wa Kings la Tatu la Kitaifa la Dijitali kuhusu kuinua mabadiliko ya dijitali Afrika, Owalo alisema kwamba serikali inatumia ICT kutoa habari na huduma kwa umma kwa kufanya rekodi za serikali kuwa za dijitali na kufanya huduma 5000 za serikali.

Alisema kwamba kupitia tovuti ya e-citizen, huduma 839 tayari zimewekwa katika tovuti huku 300 zikiwekwa kila wiki kufikia lengo la Juni 2023.




**Waziri wa Habari, Teknolojia na Uchumi Dijitali (kati) na Balozi wa Amerika nchini Meg Whitman pamoja na Afisa Mkuu Mtendaji wa Nation Media Group, Stephen Gitagama wakati wa kongamano la Nation Digital mjini Mombasa.**

"Pendekezo letu la huduma 5,000 kufikia Juni linaweza kuafikiwa. Tunalenga sekta ya kibinafsi ili tuweze kunufaisha uchumi wetu kupitia muda mfupi iwezekanavyo," alisema.

"Kama sehemu yetu ya ajenda ya dijitali kuelekea serikali isiyotumia karatasi, Afisi ya Baraza la Mawaziri na mikutano tayari zimefanywa kuwa za dijitali kwa ubora na utendaji," alisema Owalo. " Tunaendelea kuhakikisha kwamba KRA inaweza kuingilia kati na kuhakikisha tuko na rasilmali za kutosha kwa mapato yetu ya ushuru ili tuweze kupanua na kuleta watu wengi kulipa ushuru na kutia nguvu matumizi yetu ya ofisi na maendeleo," aliongeza Owalo.

Alisema kwamba mipango inaendelea kuanzisha kitambulisho cha taifa cha dijitali ambacho kitawezesha matumizi ya tekinolojia ya dijitali kutambua Wakenya kupitia mfumo wa pamoja wa rekodi kuu ya data ya raia wote.

Waziri alisema kwamba rekodi hiyo kuu ya data itatumiwa kutanbua raia, na akaongeza kuwa itawawezesha kupata huduma za serikali wakiwa nyumbani.

Waziri Owalo alisema kupanua mpango mkuu wa kitaifa wa faiba ya dijitali kwa kilomita 100,000 kwa miaka mitano ijayo kunafanywa kwa ushirikiano na sekta ya kibinafsi.

"Kwa kuwa Baraza la Mawaziri limeidhinisha, sasa tunaweza kuanzisha kilomita 5,000 za kwanza kufikia Juni 2023 na zingine zitajenga na sekta ya kibinafsi," alisema.

# Mpango mpya wa pensheni kunufaisha wastaafu nchini

ENDELEA KUTOKA UK 1

kudumu ya kulipwa pensheni.

Ni lazima wanachama wachange asilimia 7.5 ya mshahara wao wa kila mwezi na serikali iwaongezee asilimia 15.

Watumishi wa umma wamehakikishiwa kupata marupurupu yao siku 30 baada ya kustaafu.

Mkurugenzi msaidizi huyo alisema tofauti na mpango wa zamani ambao mtu alitimiza umri wa kustaafu ( miaka 60) ili aweze kupata pensheni, katika mpango wa sasa wa kuchanga wamehakikishiwa kulipwa pesa kwa pamoja hata wakistaafu mapema.

"Serikali ilikuwa na nia njema kwa kuanzisha mpango huu mpya ili kuwezesha watumishi wa umma kustaafu vyema na wakiwa na marupurupu makubwa na pia bima ya afya," alisema Bw Obonyo.

Obonyo alikuwa akizungumza mjini Homa Bay katika mkutano wa hamasisho kuhusu PSSS ambapo alisema kwamba Wizara ya Fedha ilitaka kueleza wanachama waelewe mpangilio wa mpito kutoka mpango wa zamani hadi mpya waweze kujipanga.

Bw Obonyo aliongeza kwamba kuna haja ya kueleza watumishi wa umma kilichofanya mpango huo mpya kuanzishwa.

Mdhamini wa PSSS , John Matiangi, alisema kwamba wanachama wa mpango huo pia wanaweza kuongeza michango yao akiongeza kuwa " wanaruhusiwa kuongeza michango yao hadi kiwango chochote wanachotaka kwa sababu hizo ni pesa zao wanazotaka kuwekeza ziwafaidi katika maisha yao wakistaafu.


## SHIRIKA LA KUFADHILI KILIMO

## TANGAZO LA ZABUNI

Shirika la Kufadhili Kilimo (AFC) ni Taasisi ya Fedha ya Maendeleo ya Serikali (DFI)inayomilikiwa kabisa na serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Shirika la Kufadhili Kilimo (CAP 323 ya Sheria za Kenya). AFC ina jukumu la kusaidia maendeleo ya viwanda vya kilimo na kilimo kwa kutoa mikopo na kutoa msaada wa usimamizi na kiufundi kwa walengwa wa mkopo.

Kwa hivyo shirika linaalika zabuni zilizofungwa kwa yafuatayo:

| NAMBARI YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI | UHITIMU |
|---|---|---|
| AFC/PREQ/01/2022-2023 | ZABUNI YA KUTOA HUDUMA ZA UBUNIFU NA MAWASILIANO | WAZI KWA WOTE |
| AFC/EOI/02/2022-2023 | ZABUNI YA KUTOA MAENDELEO YA MKAKATI WA MABADILIKO, KULAINISHA BIASHARA, KUCHANGISHA FEDHA NA KUELEZEA HATARI ZINAZOLIKABILI SHIRIKA | WAZI KWA WOTE |

Wazabuni wamealikwa kushiriki katika zabuni za hapo juu kwa kuwasilisha nakala ngumu za zabuni zao kwenye Sanduku la Zabuni lililoko kwenye Orofa ya 5 ya Jumba la Development, Moi Avenue, Nairobi.

Wazabuni wanaovutiwa wanaweza kupata habari zaidi kutoka Ofisi ya Ununuzi kwenye Orofa ya 6, Jumba la Development, kando ya Moi Avenue au kupitia barua pepe procurement@agrifinance.org

Hati za zabuni zinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka kwa wavuti ya shirika: www.agrifinance.org au Tovuti ya Zabuni ya Serikali ya Kitaifa www.tenders.go.ke

Zabuni zote zitafungwa **Jumatano 8 Machi 2023 saa 11.00 asubuhi** ambapo zitaandikwa nambari sahihi ya zabuni katika bahasha na kutumwa kwa:

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Kufadhili Kilimo,**
**P.O. Box 30367, 00100 GPO, Nairobi.**

Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika **Chumba cha Mikutano cha AFC/ADC Orofa ya 3, Jumba la Development.**



REPUBLIC OF KENYA

## KENYA UTALII COLLEGE

*Lango kuu kwa nafasi za kazi za kimataifa katika sekta ya Hoteli na Utalii*

## NOTISI YA TENDA

### TENDA NAMBARI KUC/43/2022/2023

### KUNUNUA, KUWEKA, KUFANYA MAJARIBIO NA KUZINDUA LIFTI KATIKA UTALII HOTEL

Kenya Utalii College inaalika maombi ya wanaotaka kushiriki kwenye tenda ya kununua, kuweka, kufanyia majaribio na kuzindua lifti moja katikaUtalii hotel.

Maelezo kamili kuhusu t5enda hizi yanaweza kupatikana kupitia lango la PPIP au Wavuti wa KUC **www.utalii.ac.ke**

Stakabadhi za Tenda zilizojazwa na kuonyesha kwenye bahasha iliyofungwa nambari ya tenda na jina kama ilivyoelezwa hapo juu inapasa kutumwa kwa: -

**The Principal & CEO**
**Kenya Utalii College**
**S.L.P 31052 – 00600 Ngara**
**NAIROBI**

Na inapasa kuwekwa kwenye Sanduku la Tenda katika eneo la mapokezi ya wageni, kabla ya saa 4.00 asubuhi mnamo siku ya mwisho; **Jumatano Machi15, 2023.** Tenda zitafunguliwa katika **Madaraka Hall** saa **4.15 asubuhi** mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wangependa kuhudhuria.

Tafadhali zingatia maagizo ya Serikali kuhusu hatua za kudhibiti maambukizi ya Covid-19. Kujipigia debe kutafanya maombi yako kutupwa nje mara moja. Piga ripoti kuhusu maswala ya ufisadi kwa: **reportcorruption@utalii.ac.ke**

**PRINCIPAL & CEO**
**KENYA UTALII COLLEGE**


ISO 9001:2015 Certified

# Undeni mitaala ya mafunzo yanayohitajika sokoni, katibu aambia TVETs

**NA DICKSON MWITI (KNA)**

Katibu wa Idara ya Serikali ya Elimu ya Kiufundi na mafunzo Anuai(TVET) Dkt Esther Muoria amehimiza taasisi za Elimu ya Kiufundi na Mafunzo Anuai (TVET) kuunda mipango itakayojaza mapengo ya ujuzi yaliyotambuliwa katika soko la leba.Akizungumza katika taasisi ya Mafunzo ya Kiufundi ya Karumo katika mahafala ya kwanza, Dkt Muoria alisema kwamba TVET imekuwa muhimu katika kuafikia ukuaji wa haraka wa kiuchumi, kijamii na tekinolojia kote ulimwenguni.

"Sababu ya hii ni kwamba wafanya kazi wanahitaji ujuzi zaidi kushiriki katika uchumi wa ufahamu. Hivyo, kwa kuwajibika taasisi za TVET zinatarajiwa kuwa mipango ya masomo inayohitajika kutoa wafanyakazi wenye ujuzi unaohitajika viwandani," alisema Dkt Muoria. Alihimiza wote wanaotoka kidato cha nne kujiunga na kozi zinazopatikana na kupata ujuzi katika taasisi za TVET, ili waweze kutimiza kazi za ndoto zao maishani.



**Dkt Esther Thaara, akitoa hotuba yake wakati wa sherehe ya kufuzu. Picha na Dickson Mwiti (KNA)**

> Nahimiza taasisi za kiufundi kuiga zile bora zaidi duniani" Dkt Muoria

"Tunafahamu kwamba wanaohitimu TVET huingia katika soko la leba lenye ushindani ulimwenguni na ni kwa sababu hii, ninahimiza taasisi zote za kiufundi kujifunza na kushirikiana na taasisi zingine kubwa ulimwenguni. Ushirikiano kama huo utatoa mipango inayotambuliwa kimataifa, inayofaa kwa soko la leba la humu nchini na kimataifa," alisema Dkt Muoria. Alisema kwamba kuna mipango ya kuanzisha mfumo wa mafunzo ya Umilisi na Utendaji (CBET), ambapo mafunzo yatakuwa yakifanywa viwandani kwa 50-50 kwa kuwa wadau wote wamekuwa sehemu ya mpango mzima. Hivyo basi alihimiza Chama cha Taasisi za Mafunzo ya Kiufundi (KATTI) kupanga upya mafunzo ya TVET kuwa ya Utendaji na Umilisi wa Ujuzi (CBS) na kutambua taasisi za kimataifa kushirikiana nazo kutoa mafunzo hayo.

Kupitia ushirikiano kama huo, aliongeza, wanafunzi wa TVET wakihitimu watakuwa wakipata vyeti mara mbili na wataweza kushindana wakitafuta kazi ulimwenguni. Alishauri wadau kuhimiza vijana kujiunga na TVET sio kwamba hawana kitu cha kufanya, lakini kwa sababu wanaweza kufaulu kwa kile watazingatia kufanya.

Mwalimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Kiufundi ya Karumo, Bi Florah Kanyua, alisema kwamba to taasisi hiyo inaendelea na mchakato wa kupata cheti cha kuidhinishwa cha ISO, kitakachowasaidia kuimarisha michakato na kufanya wateja kuridhika na hivyo basi kuwa na maendeleo endelevu.

# Nchi 18 zakutana Nairobi kuinua mipango ya kudhibiti Malaria Afrika

**NA JUDY SHERI (PCO)**

Wawakilishi kutoka nchi 18 kote ulimwenguni, wamekutana Nairobi kuchunguza mikakati ya kuharakisha kuthibiti na kuangamiza Malaria katika Afrika.

Mkutano huo, ulioandaliwa na Wizara ya Afya na Roll Back Malaria Partnership to End Malaria, ulitokana na kuongezeka kwa hofu kuhusu kukaribia kukwama kwa mipango ya kuthibiti Malaria iliyofichuliwa kata Ripoti ya Malaria ulimwenguni ya mwaka wa 2022.

Dkt Josephine Mburu, Katibu wa Afya ya Umma na Viwango vya Utaalamu katika Wizara ya Afya alifungua mkutano huo kwa kusisitiza umuhimu wa ushirikiano katika vita dhidi ya Malaria. Mapendekezo ya mkutano huo yatahakikisha usalama wa bidhaa, kuimarisha kinga, na kutia nguvu mifumo ya afya kuelekea kuangazia malaria.

Matokeo ya mkutano huo, yatasaidia kuharakisha uthibiti wa Malaria na kuangamiza hasa katika Afrika inayochangia asilimia 96 ya visa na vifo kote ulimwenguni.

Dkt Mburu alisema licha ya hatua kubwa kupigwa katika vita dhidi ya malaria, bado na mapengo katika kufikisha mpango huo, mbu kutouawa na dawa na dawa kutofanya kazi. Vile vile alihimiza mipango mikubwa ya kupanua ushirikiano wao zaidi ya nchi zao ili kuhakikisha hakuna inayobaki nyuma katika juhudi za kuzuia na kutibu malaria.

Dkt Mburu alihimiza wawakilishi hao kutayarisha mapendekezo ambayo yatalinda na kuhakikisha uendelevu. Pia alishukuru washirika wa maendeleo kwa kuendelea kutoa usaidizi na akatambua juhudi za ushirikiano wa RBM katika kumaliza malaria.

REPUBLIC OF KENYA
RBA Retirement Benefits Authority

## MWALIKO WA ZABUNI

Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu (RBA) ni shirika linalolenga wateja ambalo linajivunia katika utoaji wake wa huduma. Mamlaka inatafuta wazabuni waliohitimu kutoa/kusambaza bidhaa/huduma zifuatazo.

Mamlaka sasa inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wazabuni wanaostahiki kwa yafuatayo:-

| Nambari ya Zabuni | Maelezo ya Zabuni | Uhitimu | Kufunga |
|---|---|---|---|
| RBA/RFP/CONSED/613/1646/2023 | Utoaji Mpango wa Elimu kwa Wateja ***(Mipango ya Kustaafu)*** | Wazi | Machi 14, 2023 saa 10:00 asubuhi |

Hati na maelezo ya zabuni yanaweza kupatikana kutoka kwa **Afisi ya Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu, Rahimtulla Tower, Orofa ya 14, Upper Hill Road, Nairobi,** baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya **Ksh. 1,000.00** inayofaa kuwekwa katika akaunti ya **RBA ya KCB 110 327 5119 Tawi la Milimani**, au, kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya RBA; **http://www.rba.go.ke** bila malipo na Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP) kwenye **www.ppip.go.ke**.

Nyaraka zote za zabuni zinapaswa kuwekwa nambari za kumbukumbu za zabuni husika, na maelezo ya zabuni na zitumwe kwa; **Afisa Mkuu Mtendaji, Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu, Rahimtulla Towers, Upper Hill Road, P.O. Box 57733-00200 Nairobi**. Zabuni zote zilizokamilishwa kikamilifu zinapaswa kuwekwa kwenye **Sanduku la Zabuni kwenye Ororofa ya 14, Rahimtulla Tower, Upper Hill Road, Nairobi** ili kupokelewa kabla au tarehe zilizotajwa na baada ya hapo kufunguliwa mbele ya wazabuni/wawakilishi watakaoamua kuhudhuria.

Kwa maswali kuhusu Sekta ya Mafao ya Kustaafu au mpango wako wa pensheni tafadhali piga simu kwa RBA kwa nambari ifuatayo ya simu bila malipo: **0800720300.**

**For more, follow us on:-**

twitter: @RBA_Kenya
Instagram: rbakenya
facebook: @RetirementBenefitsAuthorityKE
linkedin: Retirement Benefits Authority Kenya
YouTube: Retirement Benefits Authority
Email: info@rba.go.ke
Website: www.rba.go.ke

***Retirement Benefits Authority (RBA) is ISO 9001: 2015 Certified***

REPUBLIC OF KENYA
KENYA WILDLIFE SERVICE

## MWALIKO WA ZABUNI

Shirika la Huduma kwa Wanyamapori Kenya limepokea fedha kutoka kwa Hazina ya Kukuza Utalii (TPF) na linataka kuwaalika wauzaji wanaovutiwa na wanaostahiki zabuni kwa yafuatayo:

| No | NAMBARI YA KUMBUKUMBU | JINA LA ZABUNI | UHITIMU | DHAMANA (KSH) | TAREHE YA KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KWS/ONT/B&F/43/2022-2023 | MAJENGO YALIYOPENDEKEZWA NA KAZI ZA KIRAIA KATIKA LANGO LA KASAALALA-MBUGA YA TSAVO MASHARIKI | WAZI KWA WOTE | 500,000/= | 10 MACHI 2023 SAA 12.00 MCHANA |
| 2. | KWS/ONT/B&F/44/2022-2023 | UCHUNGUZI WA MAJI NA JIOLOJIA, KUCHIMBA VISIMA NA KUWEKA VIFAA KATIKA LANGO LA KASAALA-MBUGA YA TSAVO MASHARIKI | WAZI KWA WOTE | 300,000/= | |

Hati za zabuni zilizo na maelezo na mahitaji ya kina zinaweza kupakuliwa bila malipo kutoka kwa wavuti yetu; **www.kws.go.ke** na Tovuti ya Ununuzi wa Umma (PPIP), **www.tenders.go.ke**.

Wauzaji wanaovutiwa wanaweza kutafuta habari zaidi kutoka Ofisi ya Kusimamia Usambazaji, Makao Makuu ya Shirika la Huduma kwa Wanyamapori Kenya kati ya saa 8.00 asubuhi na 5.00 jioni wakati wa siku za wiki, Simu. 020-2379407-15 Rununu: 0726610508/9, au barua pepe: **hps@kws.go.ke.**

Ufafanuzi wote na /au marekebisho yatachapishwa kwenye wavuti ya KWS na wauzaji wanahitajika kuangalia mara kwa mara kwa nyongeza yoyote au marekebisho wakati wa kipindi cha zabuni kabla ya tarehe ya kufunga

Zabuni zilizokamilishwa ziwekwe katika bahasha iliyofungwa iliyo na nambari ya kumbukumbu ya zabuni na jina la zabuni, itawekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililopo kwenye **Eneo Kuu la Mapokezi, Makao Makuu ya KWS, Barabara ya Langata P.O. Box 40241 - 00100, Nairobi** mnamo au kabla ya **10 Machi 2023** saa **12:00 mchana.**

Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaoamua kuhudhuria kwenye Chumba cha Mikutano cha KWS Vet.

Habari zaidi zinapatikana katika **www.kws.go.ke.**

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA HUDUMA KWA WANYAMAPORI KENYA**

**“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**




# Chuo Kikuu chazindua mradi wa kushughulikia taka ya elektroniki

**BY DICKSON MWITI (KNA)**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Meru kimezindua mradi wa kushughulikia taka na inayotokana na elektroniki kuinua utunzaji wa mazingira kwa kuondoa taka nyingi ya elektroniki nchini.Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Makamu Chansela wa MUST Profesa Romanus Odhiambo alisema kwamba mradi huo unalenga kuhamasisha umma na kuzungumza na wadau katika taka ya elektroniki kuhusu ubadilishaji, kuwapa mafunzo watu wengi iwezekanavyo na kupanua



**Naibu Chansela wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Meru Prof Romanus Odhiambo akihutubia waandishi habari chuoni humo.**

uwezo wa utengenezaji pamoja na utafiti na kuunda nafasi za ajira. Alisema kwamba taasisi hiyo tayari imewapa mafunzo mafundi 175 ambao watakuwa wakihitimu Juni na ambao watatoa ujuzi wao vijijini na hatimaye kote nchini Odhiamboalisema kwamba watakaohitimu watakuwa pia kama maajenti wa kituo cha ukusanyaji cha Chuo Kikuu hicho huku kikiendelea kuongeza mradi huo.

Kulingana na ripoti ya kufuatilia taka ya elektroniki ya mwaka wa 2020, tani milioni 53.6 milioni za taka ya elektroniki zinatolewa kila mwaka na iwapo zitaachwa bila kushughulikiwa zitaongezeka hadi tanil 20 milioni kufikia

2050. Kote ulimwenguni, ni asilimia 17.4 pekee ya taka ya elektroniki inayoshughulikiwa ipasavyo," alisema Odhiambo. Aliongeza kuwa taka ya elektroniki inatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia tano hadi asilimia nane kutokana na ongezeko la vifaa vya ICT ulimwenguni.

“Sisi ndio chuo kikuu cha kwanza nchini kubuni muundo ambao rasilmali zinatumiwa na kuwekwa kuliko kutupwa zikitimiza muda wa kutumiwa," alisema Odhiambo.

Alisema kwamba Chuo Kikuu hicho kitajihidi kuwa na uchumi unaolenga kutotoa taka na badala yake, bidhaa, vipuri na nyenzo zitakazotumiwa, zitatunzwa, kurekebishwa, kutumiwa upya na kubadilishwa iwezekanavyo katika njia bora kwa mazingira. “Hii inanuiwa kuwa njia mbadala ya uchumi unaochangia taka nyingi ya elektroniki inayotupwa," alisema Odhiambo. Mradi huo umefadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Ujerumani kwa usaidizi wa Muungano wa Ulaya na washirika wa kibinafsi yanayoshughulikia taka ya elektroniki.




**Kituo cha kushughulikia taka ya kielektroniki chuoni humo. Picha na Dickson Mwiti (KNA)**


REPUBLIC OF KENYA

KENYA Forest Service

## UFUNGUZI MPYA WA USAJILI DIJITALI WA WAWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MISITU

| | |
|---|---|
| **KUMBUKUMBU:** | **KFS/DISP/01/2022 - 2023** |
| **JINA LA ZABUNI:** | **USAJILI DIJITALI UNAOENDELEA WA WAWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MISITU (MBAO, PLYWOOD, KUNI ZA KUNDE, VIGINGI VYA KUWEKEA NYAYA VILIVYOTIBIWA NA KUNI ZA MAFUTA) KWA MIAKA YA KIFEDHA 2021/2022 – 2022/2023** |

Tunarejelea tangazo kuhusu Usajili dijitali ambalo lilitokea kwenye gazeti la My Gov mnamo tarehe 10 Agosti, 2021 na kufungwa mnamo tarehe 24 Agosti, 2021.

Hili ni kuwajulisha wawekezaji wote katika sekta ya misitu ambao hawakuwa wametuma maombi yao kufikia tarehe ya kufungwa (waombaji wapya), wale ambao walikuwa wamejiandikisha tu lakini walikuwa hawajamaliza usajili kwa sababu moja au nyingine (hawakustahiki mazoezi ya ukaguzi halisi) na wale ambao walikamilisha usajili katika mfumo lakini wakashindwa wakati wa zoezi la uhakiki halisi kwamba usajili dijitali umefunguliwa tena kwa ***siku thelathini (30) kuanzia tarehe 28 Februari 2023 na kufungwa tarehe 29 Machi, 2023, saa 12 mchana. Hii ni kuruhusu usajili unaoendelea.***

**N.B Wawekezaji wote katika sekta ya misitu ambao walifaulu kusajiliwa na wale tayari walio katika orodha yetu ya wawekezaji wa sekta ya misitu waliosajiliwa hawahitajiki kutuma maombi tena.**

Waombaji wanahitajika kutembelea wavuti ya KFS **www.kenyaforestservice.org** kupata nakala ya hati inayoongoza mchakato wa usajili na pia kufahamu vigezo vya utathmini kabla ya kuwasilisha maombi yao mtandaoni. Hati hizo pia zinaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya ununuzi wa umma **www.tenders.go.ke.**

Ili kujiandikisha, tembelea Tovuti ya Huduma ya Misitu ya Kenya- ***kichupo cha usajili*** kwa kutumia kivinjari chochote- **www.kenyaforestservice.org**

Au fungua kiunga- **https://sawmillers.kenyaforestservice.org**
Maelezo ya mchakato wa usajili yanapatikana kwenye ukurasa wa usajili dijitali.

Baada ya uwasilishaji mzuri wa maelezo ya maombi na baada ya uthibitisho katika mfumo, mwombaji ataarifiwa kuhusu hali yake ya maombi kupitia barua pepe iliyotolewa wakati wa usajili.

Baada ya kufungwa kwa usajili wa mtandaoni, maombi yote yaliyofanikiwa katika mfumo huo yatapitia uthibitisho wa habari uliotolewa katika mfumo na mwombaji.

Matokeo ya mwisho ya uthibitisho wa kawaida itakuwa orodha ya wawekezaji wa sekta ya misitu iliyosajiliwa (Mbao, kuni za kunde, vigingi vya kuwekea nyaya, kuni na kuni za mafuta) ambao wataalikwa kwa zabuni ya vifaa vya upandaji miti mara kwa mara wakati wowote zinapopatikana katika ya miaka ya kifedha ya 2022/2023.

**Usaidizi/msaada**
Kwa msaada wowote tafadhali wasiliana na KFS kupitia anwani hizi wakati wa saa za kawaida za kazi;
a) **0202020285/0202014663/0202689882**
**Au**
b) **Barua pepe: eregistration@kenyaforestservice.org**
**Au**
c) **Tembelea ofisi yoyote ya Idara ya Kusimamia Misitu**

**Mhifadhi Mkuu wa Misitu**
**Idara ya Kusimamia Misitu Kenya**

KENYA VISION 2030



REPUBLIC OF KENYA

nema

## ZABUNI WAZI KITAIFA

Mamlaka ya Kitaifa ya Kusimamia Mazingira (NEMA) inakaribisha zabuni zilizofungwa kwa zabuni zilizo wazi zifuatazo. Hati za Kina za Zabuni zinapaswa kupakuliwa kutoka kwa tovuti yetu: **www.nema.go.ke**; au tovuti ya habari ya manunuzi ya umma **www.teners.go.ke** ***bila malipo*** na kwa ada isiyoweza kurejeshwa ya Ksh.1,000 ikiwa itapatikana kutoka Sehemu ya Ununuzi ya NEMA katika **Makao Makuu ya NEMA yaliyo kando ya Barabara ya Popo, Nje ya Barabara ya Mombasa**. Ada ya zabuni inapaswa kuwa katika Hundi ya Benki au kuweka pesa taslimu katika **Akaunti ya Mapato ya NEMA, KCB - Tawi la KICC, Nambari ya Akaunti 1102298158**, na kuwasilisha hati ya amana, katika Ofisi ya Fedha kwenye Orofa ya Chini Elland House Makao Makuu ya NEMA. **Tafadhali kumbuka kuwa pesa taslimu haitakubaliwa.**
Jaza hati za zabuni katika bahasha zilizofungwa wazi na zilizowekwa alama ya **“Nambari ya Marejeleo ya Zabuni na Jina** kama ilivyoelezwa hapa chini:

| No. | MAELEZO | KUMBUKUMBU | KUFUNGA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi, upimaji na uagizaji wa mtambo uliopendekezwa wa kuondoa chumvi. ***(Imetangazwa upya)*** | NEMA/T/23/2022/2023 | Machi 15, 2023 saa11:00 asubuhi |
| 2. | Ujenzi wa kiwanda cha kupozea samaki- Kazi za kiraia, Ekakala, Kaunti ya Machakos (***Imetangazwa upya)*** | NEMA/T/25/2022/2023 | Machi 15, 2023 saa11:00 asubuh |
| 3. | Usambazaji, uwekaji, upimaji na uagizaji wa mashine ya kutengeneza vitalu vya barafu na kazi zinazohusiana na kiraia, Ndhiwa, Kaunti ya Homabay ***(Imetangazwa upya*** | NEMA/T/27/2022/2023 | Machi 15, 2023 saa11:00 asubuh |
| 4 | Huduma za ushauri kwa ushauri wa usimamizi wa maarifa kwa mpango wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Kenya | NEMA/EOI/NIE/002/ 2021-2022 | Machi 15, 2023 saa11:00 asubuh |

inapaswa kutumwa kwa:-
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Kusimamia Mazingira Kenya,**
**Eland House, Barabara ya Popo, Nje ya Barabara ya Mombasa,**
**P.O. Box 67839 - 00200.**
**NAIROBI**

Inapaswa kuwekwa katika Sanduku la Zabuni lililo katika eneo la Mapokezi la NEMA, Eland House, Barabara ya Popo, nje ya Barabara ya Mombasa ili ipokewe mnamo au kabla ya **Jumatano tarehe 15 Machi 2023 saa 11:00 asubuhi**. Zabuni kubwa zitawekwa katika Ofisi ya Ununuzi G16. Hati ya zabuni itafunguliwa katika makao makuu ya NEMA tarehe **15 Machi 2023 saa 11:00 asubuhi**. Hati zilizowasilishwa baada ya wakati huu hazitakubaliwa.

Zabuni ya yeyote atakayepatikana akidanganya au akitoa taarifa za uwongo itafutiliwa mbali.

Barua pepe: **dgnema@nema.go.ke**
**Simu: (020) 2183718, 2101370, 0723 363010, 0735 013046, 0724 253398**
Ripoti matukio na malalamiko:
Simu ya kuripoti matukio NEMA : **0786 101 100,**
**www.nema.go.ke**

***Our Environment, Our Life, Our Responsibility.***

**National Environment Management Authority - Kenya**
**@NemaKenya**
KENYA VISION 2030

Funika mdomo unapopiga chafya
20 SEC
Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza
Jitenge na walio na virusi
Usiguse macho, pua au mdomo na mikono michafu
Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi
Hakikisha maeneo yote ni safi
KOMESHA COVID-19



kasneb

Kasneb Towers, Hospital Road, Upper Hill, P.O. Box 41362-00100 NAIROBI
Landline telephone number: +254 (020) 4923000, I Cellphone: 0722-201214, 0734-600624
Email: info@kasneb.or.ke. I Website: www.kasneb.or.ke
Facebook: KASNEBOfficial I Twitter:@KASNEBOfficial

## FURSA ZA KAZI – TANGAZO LA NJE KWA NAFASI ZA KAZI

Kasneb ni shirika la serikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambalo uanzishwaji na utendakazi wake unasimamiwa na Sheria ya Wahasibu, Na. 15 ya 2008, Sheria ya Makatibu wa Umma Walioidhinishwa wa Kenya, Sura ya 534 ya 1988 na Sheria ya Uwekezaji na Wachambuzi wa Fedha, Na. 13 ya mwaka 2015.

Jukumu la kasneb ni kuandaa silabasi na kusimamia mitihani ya kiufundi, cheti, stashahada, taaluma na baada ya utaalamu. Pia inatoa vyeti kwa wagombea katika uhasibu, fedha, mikopo, utawala na usimamizi, teknolojia ya habari na taaluma zinazohusiana. Mamlaka yake ni pamoja na kukuza sifa zake kitaifa na kimataifa pamoja na kutoa vibali kwa taasisi husika za mafunzo kwa kushirikiana na Wizara inayosimamia Elimu.

Katika kutekeleza jukumu lililo hapo juu, Bodi ya kasneb inakaribisha maombi kutoka kwa Wakenya waliohitimu ipasavyo kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi:

| S. NO | NAFASI | DARAJA | IDARA | KITENGO | IDADI | NAMBARI YA MAREJELEO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mkurugenzi, Uendelezaji Mitihani | 2 | Uendelezaji wa Mtihani | N/A | 1 | HRM/DTD/2/2023 |
| 2. | Mkurugenzi, Utafiti na Maendeleo ya Mitaala | 2 | Utafiti na Maendeleo ya Mitaala | N/A | 1 | HRM/DCRD/2/2023 |
| 3. | Mkurugenzi, Usimamizi wa Mitihani na Usindikaji | 2 | Usimamizi na Usindikaji wa Mitihani | N/A | 1 | HRM/DEAP/2/2023 |
| 4. | Afisa Mkuu wa Sheria | 4 | Katibu wa Shirika na Huduma za Kisheria | Huduma za Kisheria | 1 | HRM/PLO/2/2023 |
| 5. | Afisa Mkuu wa Mitihani | 4 | Usimamizi na Usindikaji wa Mitihani | Usimamizi wa Mitihani | 1 | HRM/PEO/2/2023 |
| 6. | Afisa Mwandamizi wa Mitihani | 5 | Utafiti na Maendeleo ya Mitaala | Ukuzaji wa Mitaala | 1 | HRM/SEOC/2/2023 |
| 7. | Afisa Mwandamizi wa Mitihani | 5 | Uendelezaji wa Mtihani | Mitihani ya Ukatibu wa Mashirika | 1 | HRM/SEOC/2/2023 |
| 8. | Afisa Mwandamizi wa Mitihani | 5 | Uendelezaji wa Mtihani | Uwekezaji na Uchunguzi wa Uchambuzi wa Fedha | 1 | HRM/SEOI/2/2023 |
| 9. | Afisa Mwandamizi wa Mitihani | 5 | Uendelezaji wa Mtihani | Mitihani mingine inayohusiana na Biashara-Usimamizi wa Mikopo | 1 | HRM/SEOO/2/2023 |

**Tafadhali Kumbuka:**

(i) Tutawasiliana na waombaji watakaofaulu pekee
(ii) Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbai.
(iii) Waombaji walioteuliwa watatakiwa kuwasilisha vitambulisho halisi vyao vya Taifa; vyeti vya masomo na taaluma wakati wa usaili.
(iv) Maelezo ya Kazi yanapatikana kwenye tovuti ya kasneb (**www.kasneb.or.ke**).
(v) Wagombea watak aofaulu (yaani, wale ambao watakaoteuliwa kwa nyadhifa zilizotangazwa) watahitajika kutoa hati zifuatazo kabla ya tuzo ya ofa kwa kuzingatia Sura ya 6 ya Katiba ya Kenya, 2010:

- Cheti Halali cha Maadili Mema kutoka Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).
- Cheti cha Uidhinisho kutoka Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC).
- Cheti cha Uzingatiaji Ushuru kutoka Mamlaka ya Kukusanya Ushuru Kenya (KRA).
- Cheti cha Kibali kutoka kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELB).
- Cheti cha Uidhinisho kutoka kwa Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo iliyoidhinishwa (CRB).

**Utaratibu wa kutuma maombi**

Wagombea wanaovutiwa na waliohitimu wanapaswa kuwasilisha maombi yao kupitia kiunga **http://bit.ly/3XWMr5I** na kuambatisha barua ya maombi, wasifu wa kina, nakala zilizoidhinishwa za matokeo ya masomo, vyeti vya taaluma na masomo, kitambulisho cha taifa, shuhuda, majina na anwani za wadhamini watatu kabla ya **Jumatano, 15 Machi 2023.** Barua ya maombi inapaswa kuonyesha **"CHEO CHA KAZI NA NAMBARI YA MAREJELEO"** ya nafasi iliyoombwa na kutumwa kwa:

**Katibu/Afisa Mkuu Mtendaji**
**Kasneb**
**P.O. Box 41362 - 00100**
**NAIROBI, KENYA**

***Kasneb ni mwajiri anayetoa fursa sawa. Watu wenye ulemavu wanahimizwa kutuma maombi na watakiwa kuwasilisha nakala ya Kadi halali ya Uanachama ya NCPWD.***

**28 Februari 2023**

b=empowered

KENYA VISION 2030

---

*INVITATION TO TENDER*

REPUBLIC OF KENYA

KenGen
Kenya Electricity Generating Company PLC

## INVITATION TO TENDER

| NO | TENDER NO. | DESCRIPTION | ELIGIBILITY | TENDER CLOSING DATE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KGN-SONDU-10-2023 | Tender for supply of strategic spares for Sondu Power Station | Citizen Contractors | 21st March 2023 at 10.0 a.m. |
| 2 | KGN-SONDU-11-2023 | Tender for repair of Sondu-Sang'oro road and drainage at Sondu Power Station.<br>***There shall be a Mandatory Site Visit on 7th March, 2023 at Sondu Power Station starting at 10.00 a.m.*** | PWD Enterprise | 21st March 2023 at 10.0 a.m. |
| 3 | KGN-HYD-(Tana)-09-2023 | Tender for Supply, Installation and Commissioning of CCTV Upgrade at Tana Power Station.<br>***There shall be a Mandatory Site Visit on 7th March, 2023 at Tana Power Station starting at 10.00 a.m.*** | Citizen Contractors | 21st March 2023 at 2.00 p.m. |
| 4 | KGN-GDD-044-2023 | Tender for Supply of Turbine Spares for Olkaria II Power Station. | Open International | 21st March 2023 at 2.00 p.m. |

Interested firms may obtain further information from the office of the **General Manager, Supply Chain, Tel: (254) (020) 3666230,** Email: **tenders@kengen.co.ke** on normal working days beginning on the date of advert. The tender documents may be collected upon payment of a non-refundable fee of **KShs.1, 000.00** paid in cash or through a banker's cheque at any KenGen finance office.

The document can also be viewed and downloaded from the website **www.kengen.co.ke** and on E-procurement **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal**.

***Bidders are advised to refer to the website and on e-procurement regularly for any additional information /clarifications/addenda. Downloaded copies are FREE.***

## SUBMISSION OF TENDERS:

1. Tender documents must be submitted online through KenGen E-Procurement web portal found on the KenGen website (**www.kengen.co.ke**)

2. Bidders who are interested in this tender **MUST** ensure that they are registered in the E-Procurement Portal. Please ensure compliance to the following;
   - For suppliers registering for the first time ensure the ***"Public Procurement"*** checkbox is ticked so that the login details are sent to suppliers automatically.
   - All documents Must be uploaded to the SRM System through the **https://eprocurement.kengen.co.ke:50001/irj/portal** found at **www.kengen.co.ke**
   - Prices to be entered under item of the RFx shall be similar to be prices in the price schedule.

**Note;** Those Bidder who have submitted their bids and wish to amend them further should not click on **WITHDRAW** but click on **EDIT** to enable them amend their bid response and make appropriate changes.

Bidders who require any form of assistance on how to bid via the system are advised to download a manual from the website or may contact **eprocurement@kengen.co.ke**

**Tender Original Security** where applicable in the form and amount specified and must be delivered in plain **sealed envelope clearly labelled with the tender number and tender description** before the closing date to the following address:

**General Manager- Supply Chain,**
**Kenya Electricity Generating Company PLC,**
**9th Floor, KenGen Pension Plaza II,**
**Kolobot Road, Parklands,**
**P.O. Box 47936, 00100**
**NAIROBI**

Tenders will be opened **online** soon after the closing time in the presence of the candidates' representatives who choose to attend at KenGen Pension Plaza II, Tender opening room, 6th floor.

***N/B: KenGen adheres to high standards of integrity in its business operations.***
***Report any unethical behavior immediately to the provided anonymous hotline service.***

**1) Call Toll Free: 0800722626**
**2) Free Fax: 00800 007788**
**3) Email: kengen@tip-offs.com**
**4) Website: www.tip-offs.com**

**GENERAL MANAGER, SUPPLY CHAIN.**

KENYA VISION 2030

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Serikali, mashirika ya kijamii wakubaliana kampeni ya pamoja ya hamisisho la dijitali

NA HAMDI MOHAMUD (KNA)

Serikali na Mashirika ya Kijamii zimekubaliana kufanya kampeni ya pamoja ya kuhamasisha umma kuhusu mpango mkubwa wa kufanya huduma za usajili kuwa za dijitali. Kuundwa kwa kundi moja kuliafikiwa katika mkutano wa mashauriano kati ya serikali na wawakilishi kutoka mashirika 25 yasiyo ya Serikali yaliyojadili malalamishi kuhusu kinga na usalama wa data ambazo zitakusanywa wakati wa usajili.

Katibu wa Uhamiaji na Huduma za Raia Julius Bitok aliyeandaa mkutano huo Nairobi, alisema kwamba serikali imejitolea kusaidia kufanya huduma 5,000 kuwa za dijitali kuepuka changamoto za utekelezaji zilizoshuhudiwa katika miradi ya awali ya dijitali.


Immaculate Kassait Kamishna wa Kutunza Data ahutubu wakati wa mkutano na mashirika ya kijamii kuhusu usajili wa kidijitali


Irungu Houtghton – Mkurugenzi Mkuu, Amnesty International Kenya ahutubu wakati wakati wa mkutano kuhusu usajili dijitali.

“Tumejitolea kushirikiana na mashirika ya kijamii. Tunafahamu changamoto ambazo serikali ilipitia wakati wa kuanzisha Huduma Namba. Gharama ya kufeli ilikuwa kubwa kuepuka kutokana na maoni na mbinu tofauti. Tunataka kutembea pamoja ili kuepuka kesi na vizingiti ambazo zitakuwa na athari hasi kwa utoaji huduma,” alisema Bitok.

Katibu alikuwa akijibu hofu ya Mkurugenzi wa Amnesty International Kenya Irungu Houghton aliyetaka hakikisho kwamba kuanzishwa kunakotarajiwa kutatanguliwa na uchunguzi kuhusu data na athari zake, mfumo wa ulinzi wa data na kujumuisha kwa umma na wadau wengine.

“Tunataka kueleza umma ili ujue kinachofanyika ili uweze kushiriki kikamilifu na kutoa maoni ili mpango huo uliotangazwa na Rais utekelezwe kwa haraka, kwa kina na uadilifu kulingana na Sheria ya Ulinzi wa Data,” alisema Houghton. Kamishna wa Ulinzi wa Data ImmaculateKassait, aliyehudhuria alisema nchi itanufaika na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Data kwa kuwa itashughulikia hofu ya wawekezaji kuhusu wizi wa habari zao za kujitambulisha na usalama wa uwekezaji wao.

Kando na wawakilishi wa serikali kundi hilo litakuwa na wanachama kutoka makundi 25 ya Mashirika ya Kijamii ambayo yanafuatilia usajili wa raia na makundi ya kutetea haki za binadamu.

REPUBLIC OF KENYA

## THE NATIONAL TREASURY AND ECONOMIC PLANNING

## INVITATION TO TENDER

**TENDER FOR SUPPLY, DELIVERY AND INSTALLATION OF NEW TECHNOLOGY LICENSES, APPLICATION AND TECHNOLOGY SUPPORT SERVICES UNDER ORACLE LICENSING MANAGEMENT SERVICES (LMS)**

**TENDER NO. TNT/018/2022-2023**

The National Treasury invites sealed Tenders from eligible Candidates for the Tender for Supply, Delivery and Installation of New Technology Licenses, Application and Technology Support Services under Oracle Licensing Management Services (LMS).

A Mandatory Pre-Bid Conference shall be held with the interested Bidders on **Tuesday 7th March, 2023** at 1000 Hours, Kenyan Time through a virtual conference meeting. Invitations shall be sent to all interested tenderers who shall submit their emails to **procurement@treasury.go.ke** before 1000 Hours, Kenyan Time on **Tuesday 7th March, 2023.**

A complete set of the Tender Documents may be downloaded by interested and eligible candidates Free of Charge at **http://treasury.go.ke** or **www.tenders.go.ke.** Those who download the documents from the website must forward their particulars immediately for recording and any further clarifications and addenda to **procurement@treasury.go.ke.**

Completed Tender Documents, both ***"Original"*** and ***"Copies",*** enclosed in plain sealed envelope and marked with the Tender Number shall be addressed to: -

**The Principal Secretary,
The National Treasury,
P.O. Box 30007 00100
Nairobi**

and be deposited in the Tender Box provided at The National Treasury, Treasury Building, 6th Floor, Harambee Avenue, Nairobi, so as to be received on or before, **Tuesday 14th March, 2023 at 11.00 a.m.** Kenyan Time.

All Bid Documents must be chronologically serialized / paginated.

All Tenders must be accompanied by a Bank Guarantee of Kenya Shillings One Million Five Hundred Thousand Only ***(Kshs. 1,500,000.00)*** from a Reputable Bank in Kenya valid for 30 days beyond the Tender Validity period.

Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of the Tenderers or their representatives who choose to attend the opening at The National Treasury, Treasury Building, Harambee Avenue, Nairobi, 6th Floor, Conference Room No. 603 on **Tuesday 14th March, 2023 at 11.00 a.m.** Kenyan Time.

**HEAD, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT SERVICES
FOR: PRINCIPAL SECRETARY/ NATIONAL TREASURY**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## THE NATIONAL TREASURY AND ECONOMIC PLANNING

## GENERAL PROCUREMENT NOTICE

| | |
|---|---|
| **Government of:** | The Government of the Republic of Kenya |
| **Project/procuring entity:** | The National Treasury, Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project |
| **GPN version:** | 1.0 |
| **GPN publication date:** | 28th February, 2023 |

The Government of the Republic of Kenya has received financing from the International Fund for Agricultural Development (IFAD) towards the cost of the National Treasury, Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project and intends to apply part of the financing to payments for contracts for goods, works and services.

The procurement program for the 2022 - 2023 period will include the following:

| Procurements for 2022 - 2023 Estimated value – US $ 729,500 |
|---|
| **Procurement of goods to include:** |
| Not Applicable |
| **Procurement of works to include:** |
| Not Applicable |
| **Procurement of consulting services to include:** |
| Supply and Installation of Financial Accounting System |
| Supply and Installation of M & E System |
| Policy Reviews Documentation |
| Consultancy Services for Baseline Survey |
| Knowledge Management |
| Bank Services |
| MFBs Services |
| Agribusiness BDS Services |
| Small Holder Fin Literacy |
| Sacco Services |
| **Procurement of non-consulting services to include:** |
| Not Applicable |

Contracts for goods, works and services will be implemented according to the principles, rules and procedures set out in the current versions of the IFAD Project Procurement Guidelines and IFAD Procurement Handbook.

Specific procurement notices for contracts to be tendered under the competitive bidding procedures will be announced as they become available on selected portals, in local newspapers, and other media outlets as appropriate.

Interested eligible bidders and consultants who wish to be included on the mailing list to receive a copy of advertisements, or those requiring additional information, should send an email to the **rkfinfa@treasury.go.ke** using the subject line "GPN 1.0 for the National Treasury, Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project and indicating which of the procurement items they are interested in.

**PROJECT COORDINATOR
RURAL KENYA FINANCIAL INCLUSION FACILITY (RK-FINFA) PROJECT
FOR: PRINCIPAL SECRETARY, NATIONAL TREASURY**

KENYA VISION 2030






# Mamlaka ya kudhibiti maji yazuia wakulima kuziba mito

**NA ANN SALATON (KNA)**

Mamlaka ya Vyanzo vya Maji (WRA) imezuia wakulima kuziba mito kufuatia uhaba mkubwa wa maji kaunti ya Narok. Mwenyekiti wa Bodi ya Kitaifa ya WRA Isaac Kool alisema kwamba viwango vya maji viko katika hali ya kuonya, kumaanisha kuwa ni maji chache inayotirika katika mito na inapozibwa, hatafaidi watu wanaoishi sehemu za chini inakopitia.

Kool alisema hali ni sawa kote nchini kwa kuwa asilimia 90 ya Mito imeathiriwa vibaya na ukame unaoendelea nchini.

Alisema kwamba mamlaka imetayarisha muundo wa kupima viwango vya maji katika mito, ili iweze kushauri watu wanapovaa kuzuia maji na wakati wa kuepuka kufanya hivyo. Katika "awamu ya kijamii kibichi" mto utakuwa umejaa maji na kuzuiwa kutaruhusiwa mtu anavyotaka. Awamu ya pili ni ya 'manjano' ambayo maji huwa yamepungua na kulazimisha Mamlaka kuthibiti uzuaji wa maji. Awamu ya tatu ni ile nyekundu ambayo miti huwa imekauka na WRA huwa haikubali uzuaji wa maji.

Kool alisema kwamba mingi ya mito katika kaunti hiyo iko kati awamu ya tatu na hivyo basi maji machache katika mito hiyo yanafaa kutiririka bila kuzuiwa.

"Tunahimiza wakulima wanaonyunyuza kando ya mito kusimamisha hadi mvua ije ili kila mtu aweze kunufaika na maji yanayopatikana," alisema.

Kool alizungumza baada ya kukutana na Kamishna wa Kaunti ya Narok Isaac Masinde na maafisa wa kampuni ya Maji na Maji taka ya Narok (NARWASCO) wakiongozwa na mwenyekiti wao Moses Samante.

Kamishna Masinde alisema timu ya idara tofauti zinazojumuisha WRA, NARWASCO, na Mamlaka ya Kitaifa ya Kulinda Mazingira (NEMA) na idara ya Ndani itazunguka kuhakikisha hakuna mkulima anayenyunyuza shamba akitumia maji ya mto katika kaunti ya Narok.

Masinde alishauri watu kuepuka uharibifu kwa kutumia maji haba wanayoweza kupata wakati huu wa kiangazi.

Kwa upande wake Samante alisema kwamba kampuni yake italazimika kuthibiti maji katika mji huo ili wakazi wanaoishi katika mitaa tofauti ya mji huo waweze kunufaika na maji haba yanayopatikana.

# Kaunti zahimizwa kutenga pesa kwa mipango ya afya ya hedhi

**NA EUNICE WANJIRU (KNA)**

Serikali za kaunti zimehimizwa kutenga pesa kusaidia mipango ya kushughulikia afya ya hedhi katika mipango yao ya sekta ya afya. Balozi wa afya ya hedhi wa Jumuiya ya Uchumi ya Ukanda wa Ziwa ambaye ni Gavana wa sasa wa Busia Dkt Paul Otuoma alisema kwamba asilimia 65 ya wanawake na wasichana nchini hawawezi kumudu sodo.

Otuoma alisema kwamba njia ya pekee ya kushughulikia afya ya hedhi ni serikali za kaunti kubuni njia za kuitengea pesa katika bajeti.



**Balozi wa Afya ya Hedhi katika Jumuiya ya Uchumi Ukanda wa Ziwa ambaye pia ni Gavana wa Busia Dkt Paul Otuoma, alivalia miwani) alipohimiza kaunti kutenga fedha za kununua sodo.**
**Picha na Eunice Wanjiru.**

Alihimiza kaunti za Jumuiya ya Uchumi ya Ukanda wa Ziwa kuunda mipango mahususi ambayo itatatua changamoto za hedhi zinazokabili wanawake na wasichana katika eneo hilo.

Otuoma alisema kwamba Jumuia ya Ukanda wa Ziwa imeshirikiana na USAID kutekeleza mpango wa kushughulikia afya ya hedhi.

USAID inalenga kuharakisha usafi na afya ya hedhi kwa kuwawezesha wadau wengi ikiwemo sekta ya kibinafsi, mashirika ya kijamii, serikali na jamii lengwa kuweka msingi wa mfumo kazi wa usafi endelevu wa mabadiliko na unaomilikiwa na kaunti hizo.

Alisema kwamba mpango huo utatoa hamisisho, hasa katika jamii ambazo zina vizingiti vya kitamaduni kwa masuala ya afya ya hedhi.

Alisema kwamba ni muhimu kushughulikia mabadiliko ya tabia ya jamii na kuzisaidia kuelewa kwamba hedhi ni hali ya kibaiyolojia.

> Visa vya wasichana kukosa shule wakiwa kwenye hedhi vimeongezeka -Otuoma

Otuoma alisema kwamba mpango huo utasaidia kuhamisha wadau tofauti, waundaji sera na watoaji wa huduma kushughulikia changamoto za afya ya hedhi. Mpango huo, pia utashirikisha matabibu na watetezi wa jinsia kueleza hasa matatizo ya kujaribu kushughulikia afya ya hedhi.Aliongeza kuwa mpango huo pia utajumuisha njia bunifu za kusaidia wale ambao wanaweza kutengeneza sodo nafuu zinazoweza kutumiwa mara zaidi ya moja.

"Kuna ongezeko kukosa masomo shuleni na asilimia 60 ya wanaokosa ni wasichana wanaopata hedhi. Hii inaathiri elimu yao na uzalishaji," akasema ," Otuoma.

Magdalene Mwajuma, afisa kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Msichana Empowerment, alisema kwamba ni muhimu kuhamasisha wasichana katika shule kwa kuwapa haki ya kupata habari kuhusu afya ya hedhi. Mwajuma alisema kwamba wengi wa wasichana na wanawake hawawezi kupata sodo bora na nafuu kwa sababu ya viwango vya juu vya umasikini hasa katika maeneo ya mashambani Kenya.

Afisa huyo alisema kwamba mpango wa kushughulikia usafi wa hedhi unalenga kubadilisha dhana hasi inayohusishwa na tamaduni za kijamii na kuleta unyanyapaa kuhusiana na mzunguko wa hedhi katika jamii.

# NTSA yapanga kukodisha huduma za ukaguzi nchini

**NA ASIYA SALAT NA MWENDE MUTHONI (KNA)**

Mamlaka ya Taifa ya Uchukuzi na Usalama (NTSA) inafanya warsha za kukusanya maoni kuchunguza na kubadilisha sheria zinazohusu uendeshaji wa gari mtu akiwa mlevi na ukaguzi wa magari ili kuongeza idadi ya magari yanayofaa kuwa barabarani na kupunguza ajali.

Kwa ushirikiano na Wizara ya Barabara na Uchukuzi, NTSA imetayarisha mabadiliko katika Sheria ya Trafiki inayohusishwa mageuzi kupitia maoni inayokusanya kwa kushirikisha umma na inayotaka yyapitishwe

Mswada wa sheria wa NTSA 2022 ambao kwa sasa unaendelea kushirikishwa kwa umma, unanuia kubadilisha sheria kuruhusu shirika hilo kutafuta huduma za ukaguzi kutoka kampuni zingine kote nchini, jukumu ambalo kwa wakati huu ni la NTSA pekee.




**Mwenyekiti, National Transport, Security Authority, Aden Noor Ali akihutubia waandishi habari katika Kenya School of Government, Mombasa. Picha na Fatuma Said**

Magari mabovu yanasemekana kuwa baadhi ya sababu za ajali za barabarani ilivyofichuliwa juzi na Mamlaka hiyo (NTSA). Kufikia Desemba 31, 2022, idadi ya vifo vilivyosababishwa na ajali za barabarani iliripotiwa kuwa ya juu zaidi kwa kipindi cha mwaka mmoja ikilinganishwa na miaka iliyotangulia vikiwa jumula ya vifo 4135 vilivyotokea eneo la ajali.

Mkurugenzi Mkuu wa , NTSA, George Njau anasema kwamba shirika hilo linapendekeza kusimamishwa kwa leseni ya dereva kwa miezi sita iwapo anapatikana akiendesha gari akiwa mlevi.

Njau anasema kwamba sheria hii inatumiwa na nchi 190 chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

"Kenya imetia saini Mkataba wa Umoja wa Mataifa, hatutungi sheria ambazo ni mpya kwa Wakenya, tunacholeta hapa ni viwango vinavyotumiwa katika sekta hii na imefaulu kupunguza ajali za barabarani kwingine ulimwenguni," alisema.

> Tutahakikisha vituo vya ukaguzi vimo kwenye kila kaunti kurahisisha huduma-Ali

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema watashirikiana kwa karibu na sekta ya uchukuzi kama wahudumu ili kusaidia kutimiza viwango vya chini vya kuendesha magari kwa njia salama. Aliongeza kuwa kubadilisha cheti chochote cha ukaguzi kinachotolewa na NTSA au kituo kingine cha ukaguzi pia kutachukuliwa kama kosa chini ya sheria za trafiki zinazopendekezwa. Mwenyekiti wa NTSA Aden Noor Ali aliomba madereva kuwa waangalifu na kuhakikisha magari yao yanakaguliwa.

Kuna vituo 17 vya ukaguzi wa magari nchini kwa wakati vilivyo na uwezo wa kukagua magari ya kibiashara.

"Tunataka kuwa na kituo cha ukaguzi katika kila kaunti kufanya huduma zetu kupatikana haraka kwa sababu lengo letu ni kupunguza ajali za barabarani kwa kuhakikisha kuna magari yanayofaa kuwa barabarani," akasema Ali. Aliongeza kuwa mamlaka ya uchukuzi inataka kushirikiana kwa karibu na waendeshaji wa bodaboda na inatayarisha sheria itakayowaweka kwa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS).

KOMESHA COVID-19
“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Wasiwasi maradhi ya akili yakitumia bili ya matibabu ya Sh62 bilioni kila mwaka

**NA YOBESH ONWONG'A (MYGOV)**

Serikali ilitumia Sh62.2 bilioni kulipa bili ya matibabu na kufidia uzalishaji uliopotea kutokana na kukosa kufika kazini, kufanya kazi kwa muda zaidi na vifo vya mapema kushughulikia matatizo ya akili katika utumishi wa umma mwaka wa 2021, kulingana na Ripoti ya Wizara ya Afya ya Hali ya Uwekezaji katika Akili Kenya 2021.

Ili kushughulikia masuala haya yanayoponza uzalishaji katika Utumishi wa Umma, serikali imeweka mikakati ya kutenga pesa zaidi kwa huduma za afya ya akili katika bajeti ya 2023/2024 na kuwafunza wafanyakazi wa afya katika viwango vyote kushughulikia na kutibu matatizo hayo ambayo yamekuwa yakiongezeka.

Akizungumza akiwa Nairobi katika hafla ya kuzindua Mpango wa Watetezi wa Afya ya Akili katika Utumishi wa Umma, Waziri wa Utumishi wa Umma na Jinsia, Aisha Jumwa, alisema kwamba nchi ina mzigo mkubwa wa matatizo ya afya na akaongeza kuwa watu 410 wamepatiwa mafunzo kuhusu matatizo ya akili ili kutoka huduma za ushauri kwa watumishi wa umma kote nchini.


**Aisha Jumwa, Waziri wa Utumishi wa Umma na Jinsia, Aisha Jumwa,**

Kulingana na Sera ya Afya ya Akili Kenya (2015-2030), inakadiriwa kuwa asilimia 20-25 ya wagonjwa wanaotafuta huduma za msingi za kutibiwa na kurudi nyumbani, huwa na dalili za ugonjwa wa akili, huku takwimu za serikali zikionyesha kwamba mmoja kati ya kila Wakenya wane wanapata ugonjwa wa akili wakati fulani katika maisha yao.

> Maradhi ya akili mara nyingi husukuma wengi kwa umaskini," Jumwa

Jumwa alisema kwamba changamoto kuu kwa matatizo ya akili ni ufahamu wa chini wa magonjwa ya akili hasa, dalili za maradhi haya miongoni mwa watu wanaougua na jamii kwa jumula.

Wakili alisisitiza kujitolea kwa serikali kuwekeza katika afya ya akili na maslahi ya watumishi wa umma kwa maendeleo endelevu.

Alisema kwamba afya ya akili inaamua hali ya afya na maendeleo ya uchumi jamii ya nchi.

Mabingwa hao wa afya ya akili watapatiwa jukumu la kuelezea visa ambavyo maradhi ya akili yanaendelea kutatizwa na itikadi za kitamaduni kama laana, uchawi na kiroho badala ya kuchukuliwa kama ugonjwa unaoweza kutibiwa na kushughulikiwa ukigunduliwa na kushughulikiwa na wataalamu.

Jumwa alisema kwamba matatizo ya akili uameathiri watu, familia, jamii na nchi.

"Matatizo ya akili huwa yanasababishia watu na familia umasikini," alisema.

Waziri alisema kwamba haki za watu walio na matatizo ya akili huwa zinakiukwa kutokana na unyanyapaa na ubaguzi.

Alisema mojawapo ya changamoto kubwa ni ufahamu wa chini wa matatizo ya akili hasa, dalili za maradhi miongoni mwa watu wanaoathiriwa.

Katika majadiliano na wataalamu wa akili na mabingwa wa afya ya akili, iliibuka kuwa ukosefu wa makao wa kuzuiwa kwa watu walio na matatizo hayo kunafanyika kwa wingi na kuwa na matatizo ya akili kunaongeza kutengwa na hatari.

# Nafasi nyingi katika uchumi Baharini, Katibu aambia wakazi

**NA BERNADETTE KHADULI (KNA)**

Wafanyabiashara wamehimizwa kutafuta nafasi zinazopatikana katika uchumi wa baharini, sekta ambayo rasilmali hazijatumiwa kikamilifu.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Masuala ya Baharini, Shadrack Mwadime, alisema kwamba sekta hiyo ina nafasi katika meli za starehe na za mizigo kwa kuwa asilimia 90 ya bidhaa husafirishwa kupitia bahari.

Mwadime alisema kwamba nchi ambazo uchumi umepanuka kupitia matumizi ya rasilmali zimeweza kustawi haraka, na akahimiza wafanyabiashara zinazowekeza katika majumba kukumbatia nafasi katika sekta ya baharini.

"Kama nchi, tunaweza kutumia sekta ya meli kupata utajiri na kutatua shida ya ukosefu wa ajira ambao uko juu kwa kubuni nafasi za ajira kwa vijana ambao ni asilimia 75 ya watu wetu," alisema Mwadime.

Katibu alisema hayo alipopokea Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya CMA CGM Bw Jean Baptiste Longin, katika ofisi yake.


**Shadrack Mwadime, Katibu wa Maswala ya Meli na Baharini Picha na Kibet Cheptumo (KNA)**

Alishukuru kampuni hiyo kwa kusaidia na kuunda uwezo wa wafanyakazi katika sekta ya baharini kwa kuungana na wadau katika biashara hiyo kuwapa nafasi wanaohitimu mafunzo ya Mamlaka ya Masuala ya Baharini waweze kupata ujuzi unaohitajika.

Wakati huo huo, Mwadime alihimiza kampuni hiyo kuwazia kuajiri wanaohitimu kutoka Kenya na kuongeza idadi ya inayopatia mafunzo hadi 25 ili kuruhusu wengi kuingia katika sekta hiyo.

Alitangaza kuwa mwaka huu, nchi itachukua 12 watakaofanya vyema zaidi kutoka Bandari Maritime Academy kuwapa mafunzo hayo

LAIKIPIA UNIVERSITY
P.O. Box 1100-20300, NYAHURURU, KENYA
TEL: +254-(0) 20 2331509; Cell: +254 713-552761 vc@laikipia.ac.ke; www.laikipia.ac.ke

OFFICE OF THE REGISTRAR
(ADMINISTRATION AND HUMAN CAPITAL

**EXTERNAL ADVERTISEMENT FOR JOB VACANCY**

Laikipia University is a Public Chartered University located 11 kms from Nyahururu Town along Nyahururu -Nakuru Road and 50 kms from Nakuru along Nakuru –Nyahururu road. The University has vacancies in the positions below;

| S/NO | POSITION | Reference |
| --- | --- | --- |
| 1 | Technologist AD 8 | LU/AD/6/2/2023 (1 Post) |
| 2 | Library Assistant III AD 5 | LU/AD/7/2/2023 (1 Post) |

More information on the posts and mode of application can be found on the University website www.laikipia.ac.ke

Closing Date: **Friday 17th March, 2023.**

Applications should be addressed to:-
**The Deputy Vice-Chancellor (AF&P)**
**Laikipia University,**
**P.O. Box 1100-20300**
**NYAHURURU – KENYA**

Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

Laikipia University is an equal opportunity employer, Youths, Women and Persons with disabilities, marginalized and minority communities are encouraged to apply.

NHIF
Afya Yetu. Bima Yetu
UHC SUPA COVER
KES 500 KILA MWEZI

- Outpatient Services
- Inpatient Services
- Maternity Package
- Surgical Package
- Dialysis Package
- Radiology & Imaging
- Mental & Behavioral Health Package
- Oncology Package
- Emergency Road Evacuation
- Overseas Benefits Package



BONYEZA *155#
UJIUNGE NA UHC SUPACOVER
SASA SOTE TUKO SAWA

nhif.or.ke | @nhifkenya
CALL TOLL FREE 0800 720 601







REPUBLIC OF KENYA

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

## TENDER NOTICE

The Communications Authority of Kenya (CA) is the regulatory authority for the ICT industry in Kenya with responsibilities in telecommunications, cybersecurity, e-commerce, broadcasting, and postal/courier services. CA is also responsible for managing the country's numbering and frequency spectrum resources, administering the Universal Service Fund (USF) as well as protecting the interests of users of ICT services.

CA invites tenders from interested and competent firms to tender for the following ;-

| No. | Tender Reference | Description of tender | Closing date and time | Eligibilty |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CA/PROC/RFP/10/2022-2023 | Open National Request for Proposal for provision of Consultancy Services for development of frameworks for effective and efficient allocation of spectrum. | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 2. | CA/PROC/OT/43/2022-2023 | Open National Tender for Supply and delivery of ICT Equipment to Schools | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Reserved to Women Owned Firms |
| 3. | CA/PROC/OT/44/2022-2023 | Open National Tender for supply, delivery, installation, commissioning & maintenance of a backup and recovery solution | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 4. | CA/PROC/OT/45/2022-2023 | Open National Tender for supply, delivery, installation, commissioning & maintenance of a network and micro segmentation solution | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 5. | CA/PROC/OT/46/2022-2023 | Open National Tender for provision of cloud services for the E-board platform | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 6. | CA/PROC/OT/47/2022-2023 | Open National Tender for provision of Microsoft 365 (e3) and email security solution | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 7. | CA/PROC/OT/48/2022-2023 | Open National Tender for provision of vulnerability and endpoint detection and response (EDR) solutions | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 8. | CA/PROC/OT/49/2022-2023 | Open National Tender for Supply and delivery of Working Tools | **8th March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 9. | CA/PROC/OT/50/2022-2023 | Open National Tender for Supply and delivery of ICT Equipment | **22nd March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Reserved to Youth Owned Firms |

### EXTENSION OF TENDER CLOSING DATE

| No. | Tender Reference | Description of tender | Old Closing date and time | Extended/new Closing date and time | Eligibilty |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CA/PROC/OT/40/2022-2023 | Open National tender for the supply, delivery, implementation, training and maintenance of a broadcast networks & services quality of service (QOS) monitoring system | 8th March 2023 10:30 am (East African Time). | **15th March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |
| 2. | CA/PROC/OT/37/2022-2023 | open national **re-tender** for provision of licenses, maintenance and support for enterprise resource planning (ERP) system | 1st March 2023 10:30 am (East African Time). | **8th March 2023** at 10:30 am (East African Time). | Open to All |

The tender document can be accessed and downloaded from the Public Procurement Information Portal **http://www.tenders.go.ke** and the Authority's website: **http://ca.go.ke/about-us/do-business-with-s/open-tenders/ free of charge.**

Further, firms who download the tender documents must arrange to forward their particulars/ contacts to the Head of Procurement, Communications Authority of Kenya, through the email address **tenders@ca.go.ke** before the closing date for records and for purposes of receiving clarifications and or addendums, if any.

Any addendum, which will be issued, will be uploaded in the CA Website

Eligible bidders may also inspect and obtain detailed hard copy of the tender documents from the Procurement Division 2nd floor Wing A at CA Centre along Waiyaki Way, Nairobi, between 9am to 4pm, Monday to Friday excluding Public Holidays at a non-refundable fee of Kshs 1,000.00

Tender documents may be obtained electronically from the Website **www.ca.go.ke, https://ca.go.ke/about-us/do-business-with-us/open-tenders** or Public Procurement Information Portal (PPIP) supplier portal (**http://www.tenders.go.ke/website/tenders/index..** Tender documents obtained electronically will be free of charge.

Prices quoted should be inclusive of all taxes, **MUST** be expressed in Kenya shillings.

Duly completed tender documents should be enclosed in a plain, sealed envelope clearly marked with the tender name and reference number should be deposited in the tender box on the ground floor of the CA Centre, so as to reach on or before the closing date and time indicated above.

**The Head of Procurement**
**Communications Authority of Kenya (CA)**
**P.O. Box 14448, Nairobi 00800**
**Tel: +254 (020) 4242000/**
**Website: www.ca.go.ke**

Bids shall be opened immediately thereafter at CA Centre ground floor, meeting room 2 in the presence of the bidders' representative(s) who choose to attend.

**Head Office**
CA Centre
P.O.Box 14448
Nairobi 00800
Mobile: : 0703042000
Email: info@ca.go.ke

**Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O.Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

**Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O.Box 8041
Mombasa 80100
Mobile:0703042152
Email: cro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134 Nyeri 10100
Mobile : 0703042181
Email : cero@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke


# NBK, kaunti zatia saini mkataba wa kufadhili miradi



**Mkurugenzi katika National Bank of Kenya, Ken Ouko, na Gavana wa Mombasa Abdulswamad Shariff Nassir, wabadilishana stakabadhi ambapo benki hiyo itafadhili miradi ya maji na afya Mombasa. Picha na Michael Maluta (KNA)**

**NA FATUMA SAID NA MICHAEL MALUTA (KNA)**

Serikali ya Kaunti ya Mombasa imetia saini Mkataba wa Maelewano na Benki ya National Bank of Kenya (NBK) kutekeleza miradi inayolenga kushughulikia upatikanaji wa huduma muhimu za afya, maji na usafi kwa wakazi wa Mombasa. Mkurugenzi wa huduma za Biashara wa NBK, Ken Ouko, alishukuru Gavana wa Mombasa Abdulswamad Sharriff Nassir kwa mpango huo akisema ni kaunti ya kwanza ambayo Benki hiyo inatia mkataba wa kufadhili miradi. Ouko alisema kwamba MOU itatekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Afya wa Kaunti (HMS) ambao utatumiwa kufuatilia na kuweka rekodi za wagonjwa, maradhi wanayogunduliwa kuwa nayo, dawa na muda wa matibabu yao, akisema data zitakapowekwa kwenye, zitaweza kupatikana na hospiitali zingine katika kaunti hiyo.
" Baada ya MOU kutekelezwa, mgonjwa hatahitaji kwenda hospitali nyingine akibeba faili iliyo na habari za huduma za afya katika vituo alivyowahi kuhudumiwa," akasema," Ouko.

"Mfumo wa afya utatuwezesha kusimamia dawa katika kaunti, na kurahisishia watu wa Mombasa upatikanaji bora wa matibabu na kuhakikisha habari zilizo katika mfumo zinapatikana mara moja zikihitajika," Ouko aliongeza.

Awamu ya pili ya mkataba huo inahusu miradi ya maji na usafi (WASH), ambayo itajumuisha uwekaji wa mita za kisasa ambazo zitawezesha kaunti kufuatilia jinsi maji yanatumiwa na raia na hivyo basi kuzuia wizi wa maji.

# Serikali kutekeleza miradi yote muhimu ya ICT-Waziri

**NA JESSICA MWANGI (PCO)**

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi Dijitali Eliud Owalo amesisitiza kujitolea kwa Wizara yake kutekeleza miradi yote muhimu ya ICT ukiwemo Mpango Mkuu wa Dijitali.

Bw Owalo akizungumza alipoongoza hafla ya kutia saini kandarasi za utendakazi za mwaka huu wa kifedha kati ya Wizara yake na mashirika ya serikali yaliyo chini yake.

Katika hafla hiyo iliyoongozwa na wenyekiti na maafisa wakuu watendaji wa mashirika yote yaliyo chini ya Wizara , Bw Owalo alisema kwamba wizara yake itabadilisha yanayotizika.

Waziri alisema kwamba ufufuzi wa mashirika utaharakisha kutimiza uwezo wa kiuchumi wa muundo wa kuanzia chini, hasa kuunda nafasi za ajira kwa mamilioni ya vijana wa Kenya.

"Vile vile, ndani ya sekta ya ICT, imekubaliwa kuwa ndani ya katika utangazaji na mawasiliano ya simu, kuna mipango ya ndani inayohitaji kushughulikiwa," alisema Owalo.

" Tayari tumejitolea kwamba tutafufua Shirika Posta la Kenya, Shirika la Utangazaji la Kenya na Shirika la Habari la Kenya ambayo ysnatatizika," aliongeza Owalo. Waziri Owalo alikumbusha mashirika ya serikali kuongozwa na mfumo kazi wa sera ya kuanzia chini katika kutekeleza majukumu yao.

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Kampeni ya kuzuia mimba za matineja yazinduliwa Kajiado

NA ROP JENET (KNA)

Chama Cha Wataalamu wa Elimu Wanawake Afrika (FAWE) Kenya, kimeanzisha mradi mpya kaunti ya Kajiado unaofahamika kama 'Imarisha Msichana' unaonuiwa kupunguza mimba za matineja. Mpango huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Mastercard Foundation katika shule nane za msingi katika kaunti hiyo na unatafuta njia za kukomesha mimba za matineja na kuhimiza wasichana matineja kurudi shule kuendelea na masomo.


Wanafunzi wa mojawapo ya shule za Kajiado West. FAWEK imeanzisha mradi wa kumaliza visa vya mimba miongoni wa matineja Kajiado. Picha na Rop Janet (KNA)

Akizungumza katika hafla ya kuzindua mradi wa 'Imarisha Msichana' Mshirikishi wa mradi huo katika kaunti hiyo Nelly Naserian alisema mimba za matineja Kenya zimeongezeka hasa wakati wa kipindi cha Covid 19. Naserian aliongeza kuwa wasichana wanalazimika kuacha shule wanapopata mimba ili kujifungua na wanakosa kurudi, na hivyo basi kukatiza elimu na ndoto zao.

"Kumekuwa na ongezeko kubwa la mimba za matineja Kenya hasa katika kipit cha Covid 19. Mimba ya tineja inakatiza elimu ya msichana kwa kuwa analazimika kuacha shule na kuwanyima nafasi ya kuendeleza elimu yao na kutimiza malengo yao ya kazi," alisema.

Alisema wasichana wengi hushiriki mapenzi bila kinga kutokana na presha kutoka kwa wenzao na kutofahamu na kujiweka katika hatari ya kupata mimba za mapema na kuambukizwa Ukimwi.

Sababu zingine za mimba za matineja ni ghasia za kingono, ukosefu wa habari za kutosha za afya na huduma za uzazi, ndoa za kulazimishwa, umasikini na ukosefu wa mwongozo wa wazazi.

REPUBLIC OF KENYA

Women Enterprise Fund

## NOTISI YA TENDA

Women Enterprise Fund (WEF) ni shirika la kiserikali ambalo ni huru chini ya Wizara ya Utumishi wa Umma, Jinsia, Maswala ya Wazee na Miradi Maalumu. WEF ilianzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali 2007, kupitia Ilani ya Kisheria no.147.

Ili kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kikamilifu, Hazina inaalika mashirika ya kutoa huduma kushiriki kwenye tenda zifuatazo:

| | NAMBARI YA TENDA. | MAELEZO YA HUDUMA | WASHIRIKI | SAA NA TAREHE YA MWISHO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | WEF/ONT/05/02/2022-2023 | UTOAJI WA BIMA YA AFYA KWA MAAFISA WA NYANJANI | KAMPUNI ZA BIMA PEKEE | MACHI 7, 2023 SAA 5:30 ASUBUHI |

Wanaotaka kutuma maombi wanapasa kupakua stakabadhi za tenda kutoka kwa wavuti **www.tenders.go.ke**. na kuwasilisha maelezo yao kwa **info@wef.co.ke** kwa kumbukumbu na ufafanuzi zaidi.

Maelezo kamili kuhusu stakabadhi za tenda yamo kwenye lango la PPIP **www.tenders.go.ke**. Stakabadhi za tenda zinapasa kuwekwa kwenye bahasha iliyofungwa ikiwa na nambari ya tenda na jina la kutumwa kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**S.LP 17126-00100**
**NAIROBI.**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

MEDICAL TRAINING COLLEGE KENYA

## CHUO CHA MAFUNZO YA MATIBABU KENYA

**KMTC is an ISO 9001:2015 Certified Institution**

***CERTIFICATION BODY: Kenya Bureau of Standards (KEBS).***

## TANGAZO LA ZABUNI

Chuo cha Mafunzo ya Matibabu Kenya kinaalika kampuni zinazostahiki kwa utoaji, usakinishaji, majaribio na uanzishaji wa Maktaba ya Kielektroniki na mfumo wa hazina wa kidijitali kama ilivyoelezwa kwenye jedwali hapa chini: -

| No. | Nambari ya Zabuni | Maelezo | Dhamana ya Zabuni (Kshs) | Walengwa | Kufunga na Wakati |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KMTC/16/2022-2023 | Usambazaji, uwasilishaji, usakinishaji, majaribio na uagizaji wa maktaba ya kielektroniki na mfumo wa hazina wa kidijitali | 150,000/= | Wazi | 14/03/2023 saa 10:00 asubuhi |

Hati za zabuni zilizo na maelezo kamili zinaweza kupatikana kutoka Makao Makuu ya KMTC, Orofa ya 1 - Afisi ya Ununuzi, baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya Shilingi za Kenya elfu moja (Ksh. 1,000/=) katika hundi ya benki kwa zabuni iliyo hapo juu. Pesa haikubaliki kabisa. Hati ya Zabuni inaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti: www.kmtc.ac.ke au http://tenders.go.ke bila gharama yoyote. Wazabuni wanaonunua au kupakua hati kutoka kwa tovuti LAZIMA wasajili Zabuni zao katika Makao Makuu ya KMTC, Afisi ya Ununuzi wakati wa saa za kawaida za kazi (08:00 asubuhi - 5:00 jioni) kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa.

Nyaraka za Zabuni zilizokamilishwa, zikiwa katika bahasha zilizofungwa na zilizowekwa namba ya Zabuni husika na zisizo na viashiria vya mtumaji, **lazima** ziwasilishwe kwa njia iliyoelezwa kwenye waraka wa Zabuni na kutumwa kwa:-

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Chuo cha Mafunzo ya Matibabu Kenya**
**P O Box 30195-00100, NAIROBI**

na ziwekwe kwenye Sanduku la Zabuni lililo kwenye Lango Kuu la Jengo la Usimamizi la KMTC, Makao Makuu-Nairobi, kabla au kabla ya tarehe na saa ya kufunga iliyoonyeshwa hapo juu.

Bei zilizonukuliwa lazima ziwe halisi (V.A.T Pamoja) zikionyeshwa kwa Shilingi za Kenya na zinapaswa kusalia halali kwa siku 120 kuanzia tarehe ya kufunga ya Zabuni huku Dhamana ya Zabuni ikisalia kuwa halali kwa siku 150. Nyaraka za zabuni zitafunguliwa mara moja baadaye mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria kwenye Uwanja Mahafala Kufuzu wa Zamani.

**AFISA MKUU MTENDAJI**

Quality health training towards realization of Vision 2030

www.wasreb.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

WASREB Water Services Regulatory Board

**WATER ACT 2016 Section 77 & 139**

## TANGAZO LA UMMA

## MIKUTANO YA MASHAURIANO YA UMMA KUHUSU LESENI ZA WATOA HUDUMA YA MAJI

Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji (WASREB) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa kampuni tatu za maji kutoa huduma za maji ndani ya kaunti zao.

Maombi ya leseni yamefanywa kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya mwaka 2016 (Kifungu cha 85(1)- '***Mtu hatatoa huduma ya maji isipokuwa kwa leseni iliyotolewa na Bodi ya Udhibiti, baada ya kuwasilisha maombi na nyaraka kama Bodi. inaweza kuhitaji'.***

Kwa hiyo, kwa kuzingatia Sheria ya Maji ya mwaka 2016 Kifungu cha 139 kuhusu hitaji la lazima la mashauriano ya umma na kitu cha msingi cha WASREB chini ya Kifungu cha 70(1) cha Sheria ya Maji ya 2016 -***ulinzi wa maslahi na haki za watumiaji katika utoaji wa huduma ya maji***', tungependa kushauri kuwa mikutano ya mashauriano ya umma ifanyike katika kumbi zilizoainishwa hapa chini ili kupata maswala ya wadau kuhusu huduma zinazotolewa, masharti ya leseni na mapendekezo ya maendeleo ya huduma kuendelea.

Tafadhali kumbuka kuwa kutokana na changamoto inayoletwa na Janga la COVID 19, Watoa Huduma za Maji watafanya mikutano mseto ya mashauriano ya umma; mikutano ya ana kwa ana kwa wadau wachache na mikutano ya mtandaoni kwa wadau wengine kama ilivyoainishwa hapa chini;

| Mtoaji wa Huduna ya Maji | KAUNTI | Eneo | | Siku, Tarehe, Muda |
|---|---|---|---|---|
| Kampuni ya Majisafi na Majitaka ya Kyeni | Embu | Mkutano wa kawaida | Jengo la Kijamii la Runyenjes, Mjini Runyenjes, Embu | Machi 23, 2023 10.00 asubuhi |
| | | Kupitia Mtandao | KYEWASCO kutoa viungo | |
| Chama cha Maji cha Muthambi 4 K | Tharaka Nithi | Mkutano wa kawaida | Afisi za makao makuu ya Muthambi 4K, Marima Road, off Embu-Meru Highway, Chogoria | Machi 24, 2023 10.00 asubuhi |
| | | Kupitia Mtandao | MUTHWASCO kutoa viungo | |
| Kampuni ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Kahuti | Murang'a | Mkutano wa Kawaida | Kangema Empowerment Centre, Mjini Kangema | 31 Machi 2023 10.00 asubuhi |
| | | Kupitia Mtandao | KAWASCO kutoa viungo | |

Washiriki wanapaswa kuwa wameketi kabla ya 10.00 asubuhi. Utambulisho wa kibinafsi wa washiriki utahitajika. Wananchi katika maeneo husika wanakaribishwa kutoa mawasilisho ya mdomo na maandishi na kuuliza maswali yoyote yanayoweza kuhusiana na utoaji wa huduma ya maji katika maeneo yao.
Maoni kuhusu ombi yatatumwa kwa barua pepe kwa info@wasreb.go.ke au kutuma kwa nakala ngumu kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji,**
**Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji,**
**Jengo la NHIF, Orofa ya 5,**
**Barabara ya Ngong,**
**P.O Box 41621 -00100,NAIROBI.**

Tarehe ya mwisho ya kupokea maoni ni siku 30 baada ya kuchapishwa kwa notisi hii.

**AFISA MKUU MTENDAJI**
**BODI YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI**

KENYA VISION 2030

***Water Services for All***

# Mamlaka ya Kitaifa ya Kusimamia Mazingira

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

**Popo Road, off Mombasa Road P.O.BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya,**
**Simu: 0724253398, 0735013046 B/Pepe: dgnema@nema.go.ke Tovuti: www.nema.go.ke**

## TAARIFA KWA UMMA KUTOA MAONI KUHUSU RASIMU YA MAZINGIRA YA MKAKATI NA TAARIFA YA TATHMINI YA KIJAMII (SESA) KWA MPANGO MKUU WA HIFADHI YA NISHATI YA KENGEN (KIWANDA), OLKARIA, KAUNTI NDOGO YA NAIVASHA, KAUNTI YA NAKURU

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57 A cha Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira (EMCA) 1999, Kanuni ya 42 na 43 ya Kanuni za Tathmini ya Athari na Ukaguzi) Notisi ya Kisheria Na. 101 ya 2003, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) imepokea Rasimu ya ripoti ya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na Kijamii (SESA) ya Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Nishati ya KENGEN (Kiwanda), Olkaria, Kaunti Ndogo ya Naivasha, Kaunti ya Nakuru. Matokeo ya SEA yanatarajiwa kuunganisha mipango na programu za kisekta zilizopo ili kuanzisha mifumo ya maendeleo endelevu.

Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya (KENGEN) PLC Mmiliki wa Mpango, inanuia kuimarisha uzalishaji wa nishati ya jotoardhi ya KenGen huko Olkaria ili kuendeleza eneo la kiviwanda yaani Bustani ya Nishati (Kiwanda) katika Kitovu cha Jotoardhi cha Olkaria katika Kaunti Ndogo ya Naivasha, Kaunti ya Nakuru, Kenya. Eneo linalopendekezwa ni la ukubwa wa Hekta 1,824 na liko ndani ya ardhi ya KenGen. Mpango mkuu unaopendekezwa umepangwa kutekelezwa katika awamu nne (4) za miaka 5 kila moja huku awamu ya awali ikitarajiwa kuanza mwaka wa 2025. Hifadhi ya Nishati inatarajiwa kuwa na viwanda vikiwemo vya Mbolea; Chuma; Plastiki na Ufungaji; Bidhaa za Chuma zilizotengenezwa; Karatasi; Bidhaa za Mbao; Nguo (Sekta Inayohitaji Mvuke); Vyakula na Vinywaji (Sekta ya Kuongeza Mvuke); Nguo(Sekta nyepesi); Vyakula na Vinywaji (Sekta ya Kuongeza Mvuke); Mabohari na Vifaa; na Kusaidia Sekta ya Mwanga.

Muhtasari wa mapendekezo ya mpango wa usimamizi na ufuatiliaji wa mazingira kwa ajili ya Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Nishati ya KENGEN (Kiwanda) umeangaziwa hapa chini.

| ATHARI | HATUA ZA KUPUNGUZA |
|---|---|
| Bioanuwai na Uhifadhi wa Asili | • Ushiriki wa mwanaikolojia katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa wanyamapori katika eneo la mpango mkuu.<br>• Vivuko vya wanyamapori vitatolewa katika korido za uhamiaji wa wanyamapori na maeneo ya mtawanyiko.<br>• Utoaji wa ukuta wa mzunguko ndani ya Hifadhi ya Nishati ili kuzuia kuingia kwa wanyamapori.<br>• Uhusiano na KWS ili kuwezesha uzio wa Hifadhi za kitaifa jirani na Barabara za KEP-Longonot na KEP-Suswa ambazo zimependekezwa.<br>• Utoaji wa vivuko vya wanyamapori katika korido za uhamiaji wa wanyamapori na maeneo ya mtawanyiko.<br>• Uteuzi wa maeneo katika Hifadhi ya Nishati ili kutumika kama maeneo ya malisho ya wanajamii wa eneo hilo kwa njia iliyoratibiwa.<br>• Uhusiano na KWS na WRTI ili kuwezesha uzio wa Kitaifa wa Hell's Gate kutoa kivuko cha wanyamapori ili kuwezesha mtawanyiko wa wanyamapori.<br>• Kufuatana na Lango la Kuzimu-Mt. Mpango wa Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia wa Hifadhi za Kitaifa za Longonot, 2017-2027.<br>• Kushirikiana na KWS katika ufungaji wa hatua za usalama kufuatilia ujangili.<br>• Ushirikishwaji wa walinzi wa KWS katika kusimamia na kufuatilia trafiki katika eneo hilo jambo ambalo litahakikisha usimamizi mzuri wa ujangili.<br>• Maandalizi na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa viumbe hai.<br>• Udhibiti wa aina za mimea utaanzishwa katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Nyaraka za upotevu wa aina katika utekelezaji wa hifadhi ya viwanda.<br>• Viwanda husika na maendeleo ya miundombinu ili kuhakikisha sensa kamili juu ya chanjo ya mimea katika maeneo yao husika.<br>• Maombi ya idhini kutoka kwa KFS/KWS kwa mimea/miti yote kupandwa ili kurejesha mimea iliyopotea.<br>• Kuajiriwa kwa mtaalamu mwenye uwezo wa bioanuwai katika kuhakikisha utekelezaji kamili na ufuatiliaji wa mpango wa bioanuwai.<br>• Vifaa vya kutumika katika shughuli zote za ujenzi viondolewe uchafu k.m. vifaa vya kuosha ili kuondoa udongo unaoweza kubeba propagules za Alien Invasive Species (AIPS) kabla ya kuletwa kwenye tovuti.<br>• Matumizi ya uso wa juu wa udongo kutoka kwenye shimo la kukopa wakati wa kuchimba kokoto kwa ajili ya ujenzi wa barabara pamoja na maendeleo ya viwanda yaepukwe ili kuepuka kusafirisha propagules za AIPS kwenye maeneo mapya.<br>• Kuenea kwa AIPS kunapaswa kudhibitiwa kwa kupunguza mara kwa mara idadi ya watu na kuajiri kwa kuwa AIPS inaonekana baadaye baada ya usumbufu wa udongo.<br>• Idara ya uvuvi katika ngazi ya serikali ya kaunti na kaunti pamoja na KMFRI inafaa kushirikiana katika usimamizi wa rasilimali za samaki katika Ziwa Naivasha.<br>• Maandalizi ya mpango wa ufuatiliaji na usimamizi wa wingi wa maji ili kudhibiti matumizi ya maji katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Uchimbaji wa visima ili kutumika kama vyanzo mbadala vya maji kwa matumizi katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Maandalizi ya sera ya mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Ajira kwa watu wenye uwezo katika kuhakikisha utekelezaji kamili wa mpango wa usimamizi na ufuatiliaji wa wingi wa maji.. |
| Mabadiliko ya Mazingira na Ardhi | • Maandalizi ya mpango wa matumizi na usimamizi wa ardhi.<br>• Kuhakikisha kwamba utunzaji wa ardhi unafanywa mara moja maeneo yaliyoathirika yamekamilika;<br>• Kuhakikisha kwamba miundombinu inayotolewa katika eneo la masterplan inaendana na mandhari iliyopo;<br>• Hakikisha kwamba udongo uliovurugwa umeimarishwa mara moja kulingana na uwezekano mkubwa wa mmomonyoko wa udongo wa eneo hilo.<br>• Hakikisha uoto katika maeneo yaliyoathiriwa kwani hii itahimiza upenyezaji wa maji na kupunguza kasi ya mtiririko.<br>• Hakikisha maendeleo yanadumishwa katika maeneo yenye mteremko wa chini ya 150.<br>• Hakikisha kuwa mabwawa ya kuzuia maji yanaunganishwa katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Ajira ya timu yenye uwezo wa wataalam katika usimamizi na ufuatiliaji wa ardhi na mazingira. |

| ATHARI | HATUA ZA KUPUNGUZA |
|---|---|
| Uchafuzi | • Maandalizi na utekelezaji wa mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa hewa.<br>• Maendeleo yote ya viwanda na miundombinu yanahakikisha kuwa tathmini ya msingi ya ubora wa hewa inafanywa.<br>• Viwanda vyote katika Hifadhi ya Nishati kufanya uigaji wa utawanyiko wa hewa.<br>• Uendelezaji wa maendeleo yote ya viwanda ufanyike kwa kuzingatia mahitaji yote ya ubora wa hewa nchini hususan Kanuni za Ubora wa Hewa za mwaka 2014.<br>• Ajira ya watu wenye uwezo katika kuhakikisha utekelezaji kamili wa mpango wa usimamizi na ufuatiliaji wa ubora wa hewa.<br>• Uundaji wa mpango wa ufuatiliaji na usimamizi wa kelele na vibration ambao utatekelezwa na mtaalam mwenye uwezo.<br>• Kazi ndani ya maeneo ya makazi na pia katika makazi ya wanyamapori inapaswa kufanywa wakati wa mchana.<br>• Viwanda husika vinapaswa kuchukua modeli ya utawanyaji wa kelele kwa kituo chao.<br>• Uendelezaji wa maendeleo yote ya viwanda unapaswa kufanywa kwa kuzingatia mahitaji yote ya kelele na mtetemo nchini hasa Kanuni za EMCA Noise and Excessive Vibration Pollution (Control) Regulations, 2009.<br>• Kuandaa mpango wa ufuatiliaji na usimamizi wa ubora wa maji.<br>• Watetezi wote wa maendeleo ya viwanda na miundombinu wanahakikisha kuwa kemikali zenye uwezo wa kusababisha uchafuzi wa maji juu ya ardhi na ardhini zinadhibitiwa ipasavyo.<br>• Maandalizi ya mpango wa kukabiliana na dharura katika kudhibiti umwagikaji wa kemikali kwa bahati mbaya. |
| Usimamizi wa Taka | • Uundaji wa mpango wa ufuatiliaji na usimamizi wa taka.<br>• Viwanda husika na watetezi wa uendelezaji wa miundombinu wanapaswa kumshurutisha mkandarasi kuhakikisha mipango sahihi katika kuhakikisha uzalishaji mdogo wa taka ngumu kutokana na shughuli za ujenzi.<br>• Wakandarasi wote wawe na mfumo wa kufuatilia upotevu.<br>• Taka zote zinazozalishwa katika kazi za ujenzi zitumike tena au zitumike tena inapowezekana.<br>• Uteuzi wa mahali ambapo taka zote za ujenzi zinashikiliwa kwa siku tayari kwa kutupwa kwenye maeneo yaliyotengwa. Wakandarasi kufanyiwa ukaguzi wa kila mwezi katika kuhakikisha uzingatiaji wa usimamizi wa taka na mipango ya usimamizi wa umwagikaji.<br>• Maendeleo yote katika hifadhi ya nishati yatafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) na uchanganuzi wa msingi wa udongo ufanywe na Ukaguzi wa Mazingira wa kila mwaka (EA) kama ilivyoainishwa katika sheria. |
| Maswala ya Kijamii | • Maandalizi ya mpango wa maendeleo ya kijamii katika usimamizi wa masuala ya kijamii katika eneo hilo.<br>• Kuanzishwa kwa programu za uhamasishaji zinazohusu ujumuishaji wa jinsia, VVU/UKIMWI na kampeni za magonjwa mengine ya kuambukiza, miongoni mwa masomo mengine ya maadili.<br>• Anzisha programu za CSR miongoni mwa jamii ya Wamaasai katika kuzingatia uwekezaji katika vituo vya kitamaduni vilivyopo na uanzishaji wa vituo vingi vya kitamaduni katika kukuza na kuimarisha tamaduni za jamii ya Wamasai.<br>• Hakikisha kuwa wanawake wengi wanapewa fursa za ajira katika Hifadhi ya Nishati.<br>• Uajiri wa timu ya wataalam wenye uwezo wa maendeleo ya kijamii huwezesha usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya maendeleo ya kijamii.<br>• Muundo wa kamati ya kurekebisha mizozo.<br>• Uundaji wa ratiba ya kuwa na mabaraza ya umma katika kuhakikisha mawasiliano endelevu kati ya timu ya utekelezaji ya Hifadhi ya Nishati na jumuiya jirani.<br>• Mikutano ya kila robo na jumuiya mwenyeji. |
| Usalama na Afya Kazini | • Uundaji wa mpango wa usimamizi wa kazi, usalama na afya na ufuatiliaji.<br>• Maandalizi ya mpango wa usimamizi wa trafiki ili kuhakikisha harakati nzuri za trafiki.<br>• Utekelezaji wa OSHA, 2007 na sheria zake.<br>• Ajira ya timu ya watu wenye uwezo wanaohusika na utekelezaji wa mpango wa usimamizi na ufuatiliaji wa kazi, usalama na afya.<br>• Muundo wa kamati ya kurekebisha mizozo. |

Rasimu kamili ya ripoti ya Tathmini ya Mazingira na Kijamii ya **Mpango Kabambe wa Hifadhi ya KENGEN Nishati (Viwandani)** inapatikana kwa ukaguzi wakati wa saa za kazi kwa:

1. **Katibu,**
   **Wizara ya Mazingira, Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Misitu,**
   **Jengo la NHIF,**
   **P.O. Box 30126-00100,**
   **NAIROBI**
2. **Mkurugenzi Mkuu, NEMA**
   **Popo Road, off Mombasa Road,**
   **P.O. BOX 67839-00200, NAIROBI**
3. **Mkurugenzi wa Mazingira Kaunti**
   **KAUNTI YA NAKURU**

Nakala ya ripoti ya Rasimu ya SEA inaweza kupakuliwa kutoka kwa **www.nema.go.ke (NEMA/SEA/5/2/078)**
NEMA inawaalika wananchi kuwasilisha maoni ya mdomo au maandishi ndani ya siku thelathini (30) za kazi kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa notisi hii kwa Mkurugenzi Mkuu, NEMA, ili kusaidia Mamlaka katika mchakato wa kufanya maamuzi kuhusu SEA.
Maoni yanaweza pia kutumwa kwa barua pepe kwa **dgnema@nema.go.ke**

**MAMO B. MAMO, EBS**
**MKURUGENZI MKUU**

***Tangazo hili linafadhiliwa na mtetezi.***

ISO 9001 BUREAU VERITAS Certification
National Environment Management Authority - Kenya
@NemaKenya
KENYA VISION 2030

FEBRUARi 28, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I Toleo No. 33/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

## KVDA yazindua miradi ya ufugaji wa nyuki kukabili wizi wa mifugo

**NA EKUWAM SYLVESTER NA JUDY TOO (KNA)**

Wafugaji katika kaunti ya Pokot Magharibi wamekumbatia ufugaji wa nyuki kama chanzo mbadala cha ajira, kufuatia juhudi za Mamlaka ya Bonde la Kerio (KVDA) kukabili athari za mabadiliko ya tabia nchi na mizozo inayosababishwa na wizi wa mifugo.

Bi Lucy Maira, mwakilishi wa kikundi cha Wanawake cha Achawa huko Kodich, Kacheliba, Pokot Kaskazini alisema kwamba ukame wa muda mrefu kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi umeathiri wafugaji na wachomaji makaa ambazo ni shughuli kuu za kiuchumi katika eneo hilo.

"Watu katika eneo hili wameambua kukumbatia shughuli tofauti kuepuka hasara ya kupoteza wanyama kutokana na ukame kwa kuanza ufugaji wa nyuki ambao una mapato mazuri," alisema.

Alisema kwamba kundi lao lilipigwa jeki wakati KVDA liliwapa mafunzo kuhusu ufugaji wa nyuki na mbinu za kuvuna asali.

"Tumepatiwa mizinga ya kisasa kuongeza uzalishaji wa asali kwa kuwa mizinga hiyo inatuletea mavuno mazuri kuliko ile ya kitamaduni, tunavuna mara mbili kwa mwaka na kwa msimu, mkulima anaweza kuvuna kilo 60 hadi 100 kwa kutegemea msimu ulivyo," alisema. Katika mahojiano na Shirika la Habari la Kenya, Mkurugenzi Mkuu wa KVDA Sammy Naporos, alisema kutokana na hali ya sasa ya uchumi, shughuli ndogo kama ufugaji wa nyuki ni muhimu na akaongeza kuwa ufugaji wa nyuki katika maeneo kame ni shughuli ya maisha kama ng'ombe wa maziwa, ukulima wa kahawa na chai eneo la Kati na maeneo mengine ya Kenya.



**Wafugaji wa nyuki waandaa asali katika Kapelel Women Group Honey Bulking and Processing Unit katik Kodich Centre, Pokot North, kaunti ya West Pokot.**




**Mfanyakazi wa KVDA Irene Domo, anayesimamia kituo cha Kodich Collection Centre, akagua asali kabla ya kupelekwa kiwandani kupakiwa.**

Alisema kwamba ufugaji wa nyuki katika maeneo kame ni mbinu endelevu ya mapato kwa sababu inafanya vyema kutokana na hali ya ekolojia kama upatikanaji wa miti yenye maua na maji miongoni mwa mengine.

Naporos aliongeza kusema kwamba kuwa na mifugo wengi kama ng'ombe, mbuzi na ngamia wanaweza kufa kutokana na ukame, na wakulima wanaweza kuwapoteza kwa wingi. Lakini kwa nyuki, mvua ya wiki mbili inatosha kwa maua kuchanua na mkulima kuvuna asali ndani ya siku 90.

Vile vile, alisema mifugo ndio chanzo cha mizozo huku jamii zinazopakana zikipigana mara kwa mara kuiba ng'ombe lakini kwa ufugaji wa nyuki, watu wa jamii hizo wanaweza kuendeleza shughuli zao kwa amani kwa kuwa wezi wa mifugo hawalengi mizinga ya nyuki. " Tuko na mipango kadhaa. Tunajenga uwezo lakini changamoto tuliyo nayo ni kwamba ufugaji wa nyuki unafanywa kwa njia ya kitamaduni. Kwa hivyo ubora wa asali unaharibika. Tunawafunza wakulima jinsi ya kushughulikia asali, kujua wakati iko tayari kuvunwa," alisema.

Naporos alisema kwamba KVDA inatumia mafundi kutengeneza mizinga kwa wingi ili kutoa asali kwa wingi.

## Serikali kuanzisha National Open University of Kenya kuongeza ufikiaji

**NA MICHAEL OMONDI (KNA)**

Mipango ya serikali ya kuanzisha National Open University of Kenya imepiga hatua. Hii ni katika juhudi za kufanya elimu ya vyuo vikuu kuwa nafuu, kufikiwa na kupatikana na wanafunzi wote. Waziri wa Elimu Ezekiel Machogu anasema kwamba hatua hiyo ni miongoni mwa mabadiliko makubwa ambayo Wizara inatekeleza kutatua shida ya gharama ya juu ya elimu ya juu nchini.

"Mojawapo ya mipango mikubwa ambayo serikali inashughulikia kwa wakati huu kuinuq upatikanaji wa elimu nafuu ya chuo kikuu ni kuanzisha National Open University of Kenya.

"Kitapoanzishwa, kitafanya elimu ya juu kuwa nafuu na kupatikana na wanafunzi wote pasipo kujali waliko na kiwango chao cha mapato," alisema.

Waziri alisema hayo alipongoza mahafala ya 10 ya Chuo Kikuu cha Pwani ambapo wahitimu1203 walipatiwa digrii tofauti.

"Lengo letu ni kuhakikisha tuko na mfumo wa elimu unaoweza kupatikana, nafuu na unaofanya kazi ambao unashindana ulimwenguni na unaofaa kwa mahitaji ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa," aliongeza Machogu.

Alisema kwamba upatikanaji wa ujuzi na ufahamu ni muhimu kwa mahitaji na kutatua changamoto za jamii ya kisasa ikiwemo maendeleo ya tekinolojia, utandawazi, mabadiliko ya tabia nchi, umasikini, usalama wa mtandao na mzigo wa maradhi.

"Jukumu la vyuo vikuu katika mafunzo, utafiti na ubunifu haliwezi kuhimizwa zaidi. Hii ni sekta muhimu inayohusiana moja kwa moja na ajenda ya maendeleo ya kikanda," alisema Waziri.

Machogu alihimiza vyuo vikuu kutafuta njia za kutatua changamoto za kifedha zinazozikabili.

" Vyuo Vikuu vyetu vinafaa kutumia uwezo wao wa kindani kuepuka changamoto zinazozikumba. Changamoto zinazozikumba kwa wakati huu zinahitaji suluhu kupitia ubunifu.

"Vyuo vyetu Vikuu vinafaa, kwa mfano, kutia nguvu mipango mahususi inayochangia ajenda ya maendeleo ya kitaifa ili kuvutia wanafunzi wa humu nchini na wa kimataifa kwa mafunzo na utafiti," alisema.

Wakati huo, alihimiza taasisi hizo kuinua mwonekano wao mtandaoni na kuwekeza katika vifaa vya kimataifa na mafunzo yanayohitajka yanayoweza kuvutia wanafunzi kutoka pande zote za ulimwengu.

## KWA UFUPI

### Serikali yatenga Sh250 bilioni kupiga jeki biashara

Serikali za kaunti zimeombwa kutambua upesi ardhi ya maendeleo ya miundomsingi na washirika wa kimkakati wa maeneo ya biashara huku serikali ikilenga kupiga jeki biashara na ukuaji wa viwanda. Akisema kwamba serikali imetafuta ufadhili wa Sh250 bilioni, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Moses Kuria alisema, serikali inaendelea kutafuta washirika wa kifedha kusaidia mipango hiyo. Bw Kuria aliongeza kuwa amejitolea kufanya nchi kuwa ya viwanda ili kuunda nafasi za ajira na kuongeza Pato la nchi na akahimiza serikali za kaunti kuchukua mwelekeo sawa.

"Ninataka kushukuru Benki ya Equity kwa usaidizi wake wa kifedha na ninaomba taasisi zingine za kifedha kufuata mkondo huo. Serikali za kaunti na wawekezaji zinapaswa kutumia mifumo ya usaidizi wa kifedha kuvutia biashara ndogo na za Kati katika maeneo yao ya viwanda," alisema.

Bw Kuria alikuwa akihutubia karibu magavana 20 katika ziara ya kujifahamisha ya Tatu City na Twiga Foods kaunti ya Kiambu.. Waziri alisema mbali na Benki ya Equity na Sh 100 milioni za serikali ambazo Rais William Ruto alitangaza za kusaidia maeneo spesheli ya kiuchumi, Exim Bank pia imekubali kuongeza dola 3 bilioni zaidi kufadhili mipango ya viwanda ya Kenya. Muungano wa Ulaya (EU) na Trademark East Africa pia zimekubali kutoa ruzuku ya Euro 25 milioni kusaidia mipango hiyo. Katibu wa Viwanda Dkt Juma Mukhwana alisema kwamba Serikali iko katika mchakato wa kufanya utafiti wa Kitaifa kutambua bidhaa ambazo zinaongeza thamani kwa maeneo husika ili kupunguza ushindani humu nchini.

"Tunapaswa kuhakikisha kwamba bidhaa zinazotengenezwa katika kaunti fulani hazitengenezwi katika kaunti jirani. Tunahitaji kupata bidhaa sahihi kwa kila kaunti ili ziongeze thamani na zishindane na zinazotengenezwa katika maeneo mengine," alisema Katibu. Alisema kwamba ina uwezo mkubwa wa viwanda na akahimiza wawekezaji kuwazia kuwekeza katika sekta ya utengenezaji bidhaa.

"Tunajua changamoto tulizo nazo kama nchi ikiwemo gharama ya juu ya stima, ushuru, lakini tunazitatua," alisema.

Na *Muoki Charles (KNA)*

### Mabaharia 200,000 kuajiriwa kufikia 2027

Serikali inapanga kuajiri mabaharia 40,000 kila mwaka ikilenga kufikisha mabaharia 200,000 kufikia 2027.

Katibu wa Idara ya Masuala ya Baharini BwShadrack Mwadime alisema kwamba uajiri wa mabaharia unafungama na Ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya Bottom-Up ya serikali ili kuunda nafasi za ajira kwa vijana wasio na ajira na walio na kazi ya mapato ya chini.

"Mpango huu utakuza kikamilifu maendeleo na kufungamanisha ukarimu, uhandisi na sekta zingine na ujuzi wa ubaharia kuunda kazi nzuri," alisema Mwandime.

Katibu, ambaye alikuwa akizungumza katika ofisi yake iliyo jumba la NSSF, Nairobi alisema kwamba maono ya serikali ya kujenga ' mabaharia wa Kenya wa kuaminiwa' inanuiwa kupata Sh3.983 trilioni katika kipindi cha miaka 35.

Bw Mwandime alisema kwamba Ajenda ya Uchumi wa Baharini, ambayo inahusu sekta ndogo za uvuvi na ubaharia, itakapotekelezwa kikamilifu, itavutia uwekezaji, kukuza utengenezaji na viwanda, kuleta mapato ya ushuru na kuunda ajira nzuri na utajiri kwa raia.

Alisema kwamba kulingana na takwimu za hivi majuzi, idadi ya mabaharia humu nchini imekuwa ikiongezeka kila mwaka, akitaja ongezeko mwaka wa 2016 kuwa 1000, mwaka wa 2020 hadi 2,000, huku Februari 2023 wakifika 6,890.

Kulingana na mfumo wa uajiri wa Mamlaka ya Shughuli za Bahari, kufikia Februari 2023, idadi ya mabaharia katika meli walikuwa 488 huku wale walio katika mchakato wa kuajiriwa wakiwa 2000. Wale walio na kandarasi walikuwa 2000, waliokuwa likizoni walikuwa 980, waliokuwa kwenye mafunzo zaidi walikuwa 512 huku wale waliokuwa kati kati ya kazi wakiwa 1000.

Katibu alihakikishia wanaopata mafunzo ya kozi za ubaharia kwamba serikali itahakikisha watapata mafunzo zaidi, na akaongeza kuwa Idara ya Masuala ya Baharini iko na washirika wakutoa ufadhili wa masomo kwa wanaotaka kuendeleza kozi zao.

*Na Bernadette Khaduli (KNA)*

REPUBLIC OF KENYA
GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke